

**MUUNDO NA UAMILIFU WA CHAGIZO KATIKA VIRAI NA VISHAZI  
VYA KISWAHILI SANIFU**

**NA**

**GRACE WAIRIMU MUTAI**

**IDARA YA KISWAHILI  
CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2019**

**Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada  
ya uzamili ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.**

## **UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kikuu chochote kile kwa minajili ya shahada.

Sahihi \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_

**GRACE WAIRIMU MUTAI**

C/50/85250/2016

## **IDHINI**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu.

**DKT. P. JERONO**

Sahihi \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_

**PROF. TOM OLALI**

Sahihi \_\_\_\_\_ Tarehe \_\_\_\_\_

## **TABARUKU**

Kazi hii naitabarukia mume wangu Jackson Kiptarus Mutai na wanangu Heather, Ronnie, Blair na Hope. Mapenzi yenu, ushauri na uvumilivu mlionionyesha ulikuwa msukumo tosha wa kuniwezesha kuikamilisha kazi hii ya kiusomi.

## **SHUKRANI**

Shukrani zangu za dhati zimwendee Maulana kwa kuniwezesha kuikamilisha kazi hii. Alinipa nguvu hasa nilipopata unyonge ulionifanya nikaribie kukata tamaa. Pia alinipa siha nzuri muda huu wote nilipokuwa naifanya kazi hii. Sifa na utukufu zikurejee Muumba wangu.

Vilevile ningependa kuwashukuru watu mbalimbali walioifanikisha kazi hii. Kwanza ni kwa wasimamizi wangu Prof. Tom Olali na Dkt. P. Jerono walioifuatilia tasnifu hii kwa makini hatua baada ya hatua. Maelekezo na mawaidha yenu ya busara yalinikwamua nilipokwama katika utafiti wangu.

Pili, ninawashukuru wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Cha Nairobi kwa kunielekeza, kuniongoza na kunihimiza katika safari yangu ya kiusomi. Hawa ni pamoja na : Prof.Irube Mwangi, Prof.John Habwe, Prof. Rayya Timammy, Prof. Evans Mbutia , Prof. Mwenda Mbatiah , Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri na Mwalimu Leonard Sanja.

Pia ningependa kutoa shukrani maalum kwa wazazi wangu marehemu Bernard Mburugua Gachagua na Mary Muthoni Mburugua kwa kunilea na kunihimiza niyaendeleze masomo yangu hadi kilele cha usomi. Ndugu zangu kwa kunihimiza nisikate tamaa hadi niyafikie malengo yangu ya kiusomi. Hawa ni pamoja na Mwai, Nyawira, Githinji, Mithamo, Kariuki(Wamai), Nyaguthii na Muriithi(Kamande) Aidha ninamshukuru mume wangu na wanangu kwa kuvumilia waliponikosa nilipokuwa naishughulikia tasnifu hii.

Nawashukuru walimu ninaofunza nao katika shule ya upili ya Upper hill hasa wanaidara wa idara ya Kiswahili kwa kunihimiza niyaendeleze masomo yangu na kunisaidia kikazi ilipobidi ili niweze kuikamilisha kazi hii bila kutatizika. Hawa ni pamoja na Carol, Jeddy, Roseline, Anne, Okari na Asatsa.

Wanafunzi niliosoma nao siwezi kuwasahau. Undugu ndani na nje ya darasa ulitupa nguvu za kuendelea na safari hii ya kiusomi. Ucheshi wenu ulituwezesha kukabiliana na masomo yalipotuwia ngumu. Hawa ni pamoja na Mwanaharusi, Wafula, Ndegwa, Brigit, Rachel, Lucy, David, Fatuma, Opiyo, Iman, Mwaipaja, Tunu, Poline, Hyline, Gladys, Joseph, Kemunto, Risasi, Rosie na Polet.

## **IKISIRI**

Mada yetu ya utafiti ilikuwa uamilifu wa chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu. Tulidhamiria kuchunguza viambajengo vya aina tofauti za chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu huku tukilenga kuonyesha miundo tofauti inayowakilishwa na aina hizi za chagizo. Tulikusudia kubaini iwapo chagizo zenye miundo fulani huwakilisha majukumu yale yale ya theta au tofauti iwapo nafasi ya chagizo husika itabadilishwa katika sentensi fulani. Utafiti wetu ulitumia nadharia ya X-baa na Theta. Nadharia ya X-baa ilitumika kubainisha miundo tofauti inayowakilishwa na chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu na ile ya Theta ilitumiwa kutambua majukumu tofauti ya theta yanayowakilishwa na chagizo hizi katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu. Data iliyotumika katika utafiti wetu ilidondolewa kutoka kwa vitabu vitatu tofauti ambavyo vilihusisha sentensi zilizokuwa na kipashio chagizo ambazo zilidondolewa na kuchanganuliwa kwa misingi ya nadharia tofauti. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo na kupitia kwa vielelezo tungo. Ilibainika kuwa kipashio chagizo ambacho ni cha ziada katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu huwa na miundo tofauti iliyoundwa kwa viambajengo tofauti na kwamba chagizo hizi huwakilisha majukumu tofauti ya theta kutegemea kinafafanua kirai kipi katika sentensi. Vilevile ilikuwa wazi kuwa chagizo zilizo na muundo sawia zaweza kuwakilisha majukumu tofauti ya theta kulingana na kitenzi kinachotoa jukumu hili la theta kwacho.

## **VIFUPISHO**

N- Nomino

T- Kitenzi

V- Kivumishi

Kbn -Kibainishi

Kj- Kijalizo

Ch- Chagizo

KN- Kirai nomino

KV- Kirai kivumishi

KT- Kirai kitenzi

KH- Kirai kihusishi

KJ-Kishazi

S- Sentensi

W- Kiwakilishi

H- Kihusishi

E - Kielezi

' -Baa moja

" – Baa mbili

XP- Kirai cha kileksika

X- Kichwa cha kirai cha kileksika

Ø- Kapa

## YALIYOMO

TABARUKU .....	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI .....	v
VIFUPISHO.....	vi
SURA YA KWANZA .....	1
1.0 USULI WA MADA.....	1
1.1 TATIZO LA UTAFITI .....	2
1.2 MASWALI YA UTAFITI .....	2
1.3 MALENGO YA UTAFITI .....	3
1.4 UPEO NA MIPAKA.....	3
1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA .....	3
1.6 MISINGI YA KINADHARIA.....	4
1.6.1 Nadharia ya Theta .....	4
1.6.2 Nadharia ya X-baa .....	7
1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA.....	12
1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu chagizo .....	12
1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya Theta .....	15
1.7.3 Yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya X-baa .....	16
1.8 MBINU ZA UTAFITI .....	17
1.8.1 UKUSANYAJI WA DATA.....	17
1.8.2 UCHANGANUZI WA DATA .....	18
1.8.3 UWASILISHAJI WA DATA .....	18
1.9 HITIMISHO.....	18
SENTENSI NA VIPASHIO VYAKE .....	19
2.0 UTANGULIZI.....	19
2.1 DHANA YA SENTENSI .....	19
2.1.1 VIRAI .....	21
2.1.2 VISHAZI.....	25
2.1.3 KATEGORIA AMILIFU ZA SENTENSI.....	28
2.2 HITIMISHO.....	35
SURA YA TATU .....	36

AINA YA CHAGIZO NA VIAMBAJENGO VYAKE .....	36
3.0 UTANGULIZI .....	36
3.1 AINA YA CHAGIZO .....	36
3.1.1 CHAGIZO ZA VIRAI .....	36
3.1.2 CHAGIZO ZA VISHAZI .....	49
3.3 HITIMISHO .....	53
SURA YA NNE .....	54
MAJUKUMU YA THETA YA CHAGIZO .....	54
4.0 UTANGULIZI .....	54
4.1 MAJUKUMU YA THETA YA CHAGIZO .....	54
4.1.1 MTENDA .....	55
4.1.2 MTENDWA .....	56
4.1.3 MNUFAIKA .....	56
4.1.4 KIFAA .....	57
4.1.5 MWATHIRIWA .....	58
4.1.6 MAHALI .....	58
4.1.7 CHANZO .....	60
4.1.8 LENGU .....	63
4.1.9 WAKATI .....	64
4.1.10 NGUVU .....	65
4.1.11 MALIGHAFI .....	66
4.1.12 MAPITO .....	66
4.1.13 MATOKEO .....	66
4.2 UTUZAJI WA MAJUKUMU YA THETA .....	67
4.3 HITIMISHO .....	69
5.0 MUHTASARI .....	70
5.1 MAHITIMISHO .....	70
5.2 MAPENDEKEZO .....	71
MAREJELEO .....	73



## **SURA YA KWANZA**

### **1.0 USULI WA MADA**

Sintaksia haifai kuangaliwa kama mfumo wa kanuni tu bila kuhusisha kigezo cha semantiki. Uundaji wa sentensi katika lugha yoyote ile hulenga kuwasilisha ujumbe fulani. Iwapo sentensi zitaundwa kwa kuzingatia kanuni pekee, uundaji huu utaweza kuzalisha sentensi ambazo si sahihi kisarufi. Gruber (1970) anasema kuwa taratibu za kuunda sentensi huzingatia umuhimu wa kisintaksia na ule wa kisemantiki. Utafiti wetu ulilenga kuchunguza namna utaratibu wa kisintaksia unahusiana na ule wa kisemantiki. Tulinuia kuchunguza viambajengo vya chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu kwa kutaka kujua ni vipashio vipi katika sentensi za Kiswahili sanifu vitatumika kukipatia kipashio chagizo majukumu ya theta. Pia, tulidhamiria kuchunguza iwapo chagizo iliyo na muundo sawa lakini ikajitokeza kwenye aina tofauti za virai ina majukumu yanayofanana au yaliyo tofauti yale ya theta.

Jerono (2003) anafafanua chagizo kama kipashio cha kikategoria ambacho hutumika kuelezea na huwa ni vile vipashio vya kielezi ambavyo mara nyingi huwa vielezi na vihusishi. Japo tunakubaliana na maoni haya, maoni yetu ni kuwa chagizo si lazima kiwe kipashio kilicho na vielezi pekee bali chaweza kuwa kipashio chochote kile ambacho kikitolewa katika sentensi husika maana ya sentensi hii haitaathirika.

Waihiga na Kagwa (2006) wanasema kuwa chagizo ni vielezi au kirai kielezi kinachotokea katika tungo lolote lile. Aghalabu hutokea baada ya kitenzi, japo si lazima kwani chaweza kutokea mahali popote au kwenye kirai chochote kile. Maoni yetu yanakubaliana na yao kwa kuwa tunasema kwamba chagizo ni kipashio cha kielezi kinachoweza kutokea kwenye kipashio chochote cha kisintaksia kama vile kirai au kishazi.

Obuchi na Mukhwana (2015) nao wanaelezea chagizo kama neno au kikundi cha maneno kinachojaza nafasi ya kielezi au vielezi. Wanadai kuwa chagizo chaweza kutokea tu baada ya kitenzi au shamirisho na ni kiambajengo cha kikazi kinachofafanua kiarifu kwa kutaja jinsi, lini na wapi. Japo maoni yetu yanakubaliana na mawazo yao, tunadai kuwa si lazima chagizo kitokee tu baada ya kitenzi kwani chaweza kutokea baada ya virai vinginevyo.

Utafiti huu uliyatumia maoni ya Lyons (1968) aliyeelezea chagizo kama kipashio cha ufafanuzi kinachofungamanishwa na kirai fulani na ambacho kinaweza kuondolewa pasi na kuathiri sentensi kisintaksia na kuwa chagizo chaweza kuingizwa katika makundi tofauti kutegemea majukumu yake ya kisemantiki. Hii ni kwa kuwa tulitaka kubaini iwapo chagizo katika Kiswahili sanifu kinaweza kufungamanishwa na kirai chochote kile au hufangamanishwa na kirai kitenzi tu pekee. Maoni haya yalitumika kuchunguza ikiwa yangeweza kutumika kuelezea chagizo cha Kiswahili na vilevile kuchunguza majukumu tofauti ya theta yanayohusishwa nacho.

Tulitumia nadharia ya X-baa kuchunguza miundo mbalimbali ya chagizo katika virai na vishazi tofauti vya Kiswahili sanifu na nadharia ya Theta kuchunguza majukumu tofauti ya theta Tulijikita kwa vipashio vinavyotoa majukumu haya ya theta kama vile vitenzi na vihusishi.

### **1.1 TATIZO LA UTAFITI**

Wataalamu wengi wameyaelezea majukumu ya kisarufi ya kipashio chagizo kwa kutumia majukumu ya kisarufi ya kielezi au kirai kielezi kama vile: namna, wakati, idadi na mahali. Aghalabu kielezi au kirai kielezi kinachotekeleza majukumu haya ya kisarufi hufafanua kitenzi na kivumishi. Tulilenga kubaini iwapo kipashio chagizo ni kipashio kinachoweza kufungamanishwa na kirai chochote na ikiwa kinawakilisha uamilifu tofauti na majukumu yale ya kisarufi ya namna, idadi, wakati na mahali katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulilenga kubaini namna majukumu ya theta yanavyotolewa kwa chagizo na namna chagizo huweza kupewa majukumu tofauti ya theta iwapo nafasi yake itabadilishwa katika muundo wa sentensi.

### **1.2 MASWALI YA UTAFITI**

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- i) Je, chagizo katika Kiswahili sanifu kina viambajengo vipi?
- ii) Je, kipashio chagizo kinawakilisha majukumu yepi ya theta katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu?
- iii) Majukumu ya chagizo yatabadilika iwapo nafasi ya chagizo husika itabadilika katika sentensi fulani?

### **1.3 MALENGO YA UTAFITI**

Utafiti wetu ulikuwa na malengo yafuatayo:

- i) Kuchunguza viambajengo vya chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu kwa mujibu wa nadharia ya X-baa.
- ii) Kubaini nafasi mbalimbali zinazochukuliwa na chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu sentensi zinapofanyiwa mageuzi ya kimuundo.
- iii) Kuchunguza majukumu ya theta ya chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu.

### **1.4 UPEO NA MIPAKA**

Tulijikita katika kuchunguza uamilifu wa chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu kwa kuhusisha vishazi huru, vishazi vitegemezi na virai vyote vya Kiswahili sanifu. Tulionyesha muundo wa chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya X-baa. Tilitumia nadharia ya Theta kubaini majukumu ya theta yanayowakilishwa na chagizo virai na vishazi.

### **1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA**

Mtafiti aliteua mada hii kwa kuwa alitaka kubaini iwapo kuna kipashio kingine cha kimuundo katika Kiswahili sanifu kinachoweza kupokea majukumu tofauti ya theta isipokuwa nomino au kirai nomino. Alikusudia kuchunguza namna vipashio vya kisintaksia vinavyoingiliana na vile vya kisemantiki kwa kutumia chagizo. Alinua kuchunguza namna chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu kinavyoweza kuchangia usahihi wa sentensi zinazotungwa na mtumizi wa lugha ya Kiswahili. Kazi hii itakuwa ya manufaa kwa watafiti wengine watakaotaka kufanya uchunguzi kuhusu uhusiano uliopo kati ya muundo wa vipashio tofauti vya kisintaksia na vile vya semantiki. Vilevile itasaidia watumizi wa lugha ya Kiswahili kufahamu umuhimu wa chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu japo ni kipashio cha ziada na kwa hivyo kuukuza ufahamu wao wa lugha hii. Pia utakuwa ni nyongeza kwa hazina ya tafiti zilizofanywa katika lugha ya Kiswahili.

## **1.6 MISINGI YA KINADHARIA**

Tulitumia nadharia ya Theta iliyoasisiwa na Gruber (1965) na Fillmore (1968). Mawazo ya Fillmore(1968) yaliyotumika katika utafiti huu ni kwa mujibu wa Newmeyer (1986). Yalitumiwa kubaini uamilifu wa chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu. Tulitumia nadharia ya X-baa kwa mujibu wa Radford (1988) ili kuonyesha muundo wa chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu.

### **1.6.1 Nadharia ya Theta**

Nadharia ya Theta inaonyesha uhusiano uliopo kati ya majukumu ya virai nomino na kitenzi kiarifu. Jukumu muhimu likiwa ni kuonyesha namna ambavyo kirai nomino kinaweza kupokea jukumu la theta kutoka kwa kitenzi. Waasisi wa nadharia hii ni Gruber (1965) na Fillmore (1968). Gruber (1970) anadai kuwa ni nadharia inayolenga kuonyesha jinsi kigezo cha kisintaksia kinavyohusiana na kigezo cha kisemantiki katika lugha. Anaongezea kuwa kitenzi ndicho kipashio muhimu kisintaksia kwa sababu kinatumiwa kubashiri majukumu ya theta ya virai nomino. Maoni haya yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwani yalituwezesha kuyabashiri majukumu ya theta yanayotolewa na vitenzi tofauti kwa chagizo ambazo zina nomino au virai nomino kwenye muundo wake.

Kulingana na Radford (1988) kategoria leksika zinastahili kuongeza habari za mahusiano dhamirifu (majukumu ya Theta) kwa habari za sifa za kategoria na sifa za uteuzi wa vijalizo. Akiwanukuu waandishi wengi wa awali walioshughulikia nadharia ya Theta akiwemo Gruber (1965) ,Fillmore (1968) na Jackendoff (1972) anasema kuwa kila agumenti ya kiarifu sharti iwe na jukumu fulani dhamirifu. Majukumu ya theta yanaweza kutumiwa kuonyesha kufanana au kutofautiana kwa vipashio katika sentensi kusikoonekana kupitia kwa muundo wa vipashio hivi.

Utafiti huu uliyatumia mawazo ya Fillmore (1968) kuchunguza majukumu ya theta ya chagizo katika virai na vishazi vya kiswahili sanifu kama yalivyoelezewa na Newmeyer (1986) aliyedai kuwa Fillmore alianzisha kiunzi cha kisintaksia kilichojumlisha majukumu ya kisemantiki aliyoyaita majukumu ya theta. Alidai kuwa majukumu haya hutolewa na kitenzi na huwa bia. Asili yake ilikuwa ukweli kuwa kiunzi kilichojumlisha viambajengo kilishindwa kuonyesha sifa za

kategoria na habari za majukumu ya theta mtawalia. Kiunzi cha viambajengo hakingeonyesha kuwa kipashio kama vile *ndani ya nyumba* ni kirai kihusishi kinachoonyesha mahali fulani.

Kwa mujibu wa Fillmore (1968) orodha ifuatayo inawakilisha majukumu ya theta yaliyo bia.

- a) Mtenda ni jukumu linalopewa kitu au mtu anayesababisha kitendo kutendeka kwa hiari
- b) Mtendwa ni uamilifu unaopewa kipashio kinachopokea athari zinazosababishwa na mtenda.
- c) Nguvu ni uamilifu unaopewa kipashio kinachosababisha kitendo fulani na kitu hiki hakionekani kwa uwazi.
- d) Kifaa ni uamilifu unaorejelea kifaa kinachotumiwa kutekeleza kitendo fulani. Sharti uamilifu huu ujitokeze pamoja na ule wa mtenda.
- e) Chanzo ni uamilifu unaotekelezwa na nomino zinazorejelea mahali au wakati ambapo jambo fulani litaanza. Aghalabu uamilifu huu hutumika pamoja na uamilifu wa lengo.
- f) Matokeo ni jukumu ambalo linawakilisha nomino inayozaliwa na kitenzi au tukio fulani.
- g) Lengo ni jukumu linalowakilishwa na mahali ambapo tendo au tukio fulani linamalizikia. Aghalabu hutumika pamoja na jukumu la theta la chanzo.
- h) Mwachiriwa ni jukumu la nomino ambayo inaathiriwa na tendo au tukio. Awali Fillmore aliliita jukumu hili la theta mtendewa.
- i) Mahali ni jukumu la theta la pahali ambapo tendo au tukio fulani linatukia.

Hata hivyo ilipolazimu utafiti huu ulitumia maoni ya Habwe na Karanja (2004) ili kubaini majukumu ya Theta ambayo hayakufafanuliwa na Newmeyer (1986) kutuwezesha kufanya uchunguzi wa kina. Majukumu haya ni:

- j) Mnufaika ni jukumu linalowakilisha agumenti inayopata manufaa kutoka kwa tukio fulani.
- k) Wakati ni jukumu linaloonyesha wakati wa kufanyika kwa tendo pasi kuhusisha na chanzo au lengo.
- l) Malighafi ni jukumu linaloonyesha bidhaa zilizotumiwa kufaulisha kitendo.
- m) Mapito ni jukumu linaloonyesha mahali ambapo nomino fulani ilipitia ikielekea mahali pengine.

Mbali na kuonyesha majukumu ya theta ya vipashio, nadharia ya Theta hujihusisha na kubaini jinsi majukumu haya ya theta huzalishwa na vipashio tofauti katika sentensi. Cowper (1992) anasema kuwa maana ya kitenzi ikijulikana, mahusiano dhamirifu yatakayozalishwa na nomino zitakazotumiwa pamoja na kitenzi hiki yatajulikana. Kwa mfano katika sentensi:

1) *Sue alikula lile tufaha*

Vipashio vya kileksika vya kitenzi *-la* vitakuwa:

*KN1 kula KN2*

*KN1: mtenda*

*KN2 :mtendwa*

Kitenzi *kula* kitachukua nomino mbili: moja katika kiima na nyingine kama yambwa. KN kabla ya kitenzi kitapewa jukumu la theta la mtenda na KN baada ya kitenzi kitapewa jukumu la theta la mtendwa. Kanuni hizi za kitenzi *kula* zaweza kuandikwa kama ifuatavyo:

*la ( mtenda,mtendwa)*

Cowper (1992) anaongezea kuwa uhusiano kati ya virai nomino katika sentensi na mahusiano dhamirifu si wa moja kwa moja. Kirai nomino kimoja chaweza kuwa na mahusiano dhamirifu zaidi ya moja. Mahusiano haya dhamirifu yanazalishwa na ubainishaji mwafaka wa kipashio cha kileksika kinachotoa jukumu fulani la theta. Jukumu la theta la KN fulani haliwezi kubashiriwa kwa kukiangalia KN husika ila jukumu la KN hueleweka tu kwa kuelewa maana ya kitenzi kinachotoa jukumu hili. Utafiti huu ulichunguza ni vipashio vipi vya kileksika vinavyotumiwa kutoa majukumu ya theta kwa chagizo na ulionyesha kipashio chagizo katika virai na vishazi kina majukumu mangapi ya theta yanayotolewa kwacho na vitenzi.

Kuiper na wengine (2014) wanasema kuwa majukumu ya theta hutolewa na vipashio tofauti vinavyohusika na utoaji majukumu ya theta ambavyo ni vitenzi, vihusishi na baadhi ya viambishi katika vitenzi lakini nomino na vivumishi havina uwezo wa kutoa majukumu haya ya theta.

Majukumu ya theta ya kipashio fulani hutolewa kwa kipashio hiki kikiwa katika nafasi fulani. Jukumu moja la theta hutolewa na kipashio kimoja kwa nafasi moja. Nadharia ya theta hivyo basi inahusu idadi ya majukumu ya theta yatakayotolewa na kipashio fulani (Cowper 1992:58) Anaongezea kuwa kila kipashio cha kileksika kitakuwa na sehemu tatu ambazo ni:

- a) Kategoria ya kipashio
- b) Sifa za kategoria
- c) Mfumo wa theta

Kufuatia haya, kitenzi weka kitakuwa na habari zifuatazo:

*Weka:* [+T - N]

[+KN KH]

[Mtenda, lengo, mahali] (Cowper 1992:61)

Hii inaonyesha kuwa sifa za kileksika za kitenzi *weka* ni kitenzi wala si nomino. Kitenzi hiki huwa na kirai nomino kama kiima na kirai kihusishi kama chagizo au yambwa. Kirai nomino kinapewa jukumu la theta la mtenda ilhali kirai kihusishi chaweza kupewa jukumu la theta la lengo au mahali.

Katika kategoria leksika, mfumo theta ni habari muhimu inayofaa kuwepo. Mfumo theta katika lugha ni mfumo unaotumiwa kutoa majukumu ya theta kwa agumenti na mfumo huu una madai yafuatayo:

- a) Katika umbo ndani, kila KN kinachorejelewa sharti kipokee jukumu la theta. Sentensi iliyo na KN kisichopokea jukumu la theta si sahihi kisasrifi.
- b) KN hupokea jukumu la theta mara moja tu.
- c) Jukumu linalopokelewa na KN fulani lafaa kudumishwa hata KN husika kinapofanyiwa mageuzi kwa kusongezwa.

Kigezo hiki cha theta kinaweza kutumika kwa umbo nje na umbo ndani. Kinapotokea katika umbo ndani, KN chochote sharti kiwe kwa nafasi iliyo na jukumu la theta. Kinapotumika katika umbo nje hakuna KN kinachoweza kusonga kwenye nafasi isiyo na jukumu la theta kwa kuwa KN husika kitakuwa na majukumu zaidi ya moja ya theta.

### 1.6.2 Nadharia ya X-baa

Nadharia ya X-baa ni nadharia iliyotangulizwa na Chomsky (1970) ili kujaribu kuunda nadharia ambayo ingeweza kudhibiti miundo virai. Fafanuzi zingine za Nadharia ya X-baa zilitolewa na Jackendoff (1974, 1976, 1977). Waasisi wa X-baa waligundua kuwa sarufi miundo virai haikukubali kategoria zaidi ya mbili. Ilibeba kategoria kirai na kategoria leksika pekee. Walidai kuwa ingewezekana kuwa na kategoria ya katikati, kati ya kategoria leksika na kategoria kirai. Massamba (2014) anaelezea kirai kama kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini

hakina uhusiano wa kiima-kiarifu (yaani hakihusishi mtendaji wa tendo na tendo lililotendwa). Ufafanuzi tulioutumiwa katika utafiti huu ni ule wa Radford (1988). Anadai kuwa nadharia ya X-baa inaongozwa na dhana ya kichwa cha kirai. Kichwa cha kirai aghalabu huwa na uhusiano fulani na maneno mengine katika kirai husika. Alama ya X huwakilisha neno kuu katika kirai husika nayo alama ( ' ) huwakilisha vipashio vifuatilizwa vya neno kuu na XP ni kirai cha X au X".Kategoria X huwakilisha kategoria za kileksika ambazo ni nomino, kivumishi, kitenzi, kihusishi na kielezi. X' ni mvurumisho wa baa moja wa X, X" ni uvurumishaji wa baa mbili ulio wa juu kabisa. X' huwakilisha vijalizo na chagizo za kichwa X. Matei (2008:219) anadai kuwa kijalizo ni kipashio kinachotumiwa kukamilisha kipashio kingine katika sentensi ilhali Lyons (1968) anaeleza chagizo kama kipashio cha ufafanuzi kinachofungamanishwa na kichwa cha kirai kinachokitegemea.

Radford alitumia alama saidizi ya X, X<sup>1</sup> (ya tarakimu) na X' (ya baa) kama njia tatu tofauti za kuelezea jambo lile moja. Radford (1988) alitumia alama saidizi ya X'. Alidai kuwa kuna viwango vitatu vya kuchanganulia virai:

i) Kiwango cha kategoria ya neno kama vile :

N-nomino

T-kitenzi

E-kielezi

H-kihusishi

V-kivumishi

ii) Kiwango cha kategoria ya kati kama vile:

N' –nomino ya baa moja

V' - kivumishi cha baa moja

T' – kitenzi cha baa moja

E' - kielezi cha baa moja

H'-kihusishi cha baa moja

iii) Kiwango cha kirai kamili kama vile :

KN –kirai nomino

KT-kirai kitenzi

KV-kirai kivumishi

KE-kirai kielezi



### KH-kirai kihusishi

Anadai kuwa kiwango cha kati huwa kikubwa kuliko kiwango cha neno na kidogo kuliko kirai kikuu. Mifano katika kirai nomino kuna viambajengo vilivyo vikubwa kuliko nomino na vidogo kuliko kirai nomino. Hali huwa hivi katika virai vingine vyote ( Radford 1988:227)

- i) Virai vihusishi vitakuwa na viambajengo vikubwa kuliko kihusishi lakini vidogo kuliko kirai kihusishi.
  - ii) Virai vivumishi navyo vitakuwa na vipashio vikubwa kuliko kivumishi na vidogo kuliko kirai kivumishi.
  - iii) Virai vielezi vitakuwa na viambajengo vilivyo vikubwa kuliko kielezi na vidogo kuliko kirai kielezi.
  - iv) Virai vitenzi pia vitakuwa na viambajengo vilivyo vikubwa kuliko kitenzi na vidogo kuliko virai vitenzi. Mifano katika sentensi
- 2) a) Yule mwanafunzi wa sintaksia [ kwmwenye nywele ndefu] amepita mtihani  
b) Alianguka<sub>[KH nje ya nyumba yake]</sub>  
c) Mkulima huyo alitota sana [ mvua iliponyesha jana]


Viambajengo vilivyo kwenye mabano katika sentensi (2) ni chagizo zilizo na miundo tofauti kama vile:

- a) *mwanafunzi = N nomino (kichwa)*  
*mwanafunzi wa sintaksia = N' (kirai cha kati)*  
*yule mwanafunzi wa sintaksia mwenye nywele ndefu = N'' (kirai kamili)*
- b) *nje ya = H kihusishi(kichwa)*  
*nje ya nyumba = H' (kirai cha kati)*  
*nje ya nyumba yake = H'' (kirai kamili)*

Kutokana na mifano (a) na (b) ni wazi kuwa kila kategoria ya kirai ina kategoria leksika kama kichwa chake. Kirai nomino kina nomino, kirai kihusishi kina kihusishi, kirai kielezi kina kielezi, kirai kivumishi kina kivumishi nacho kirai kitenzi kina kitenzi. Kipashio ambacho ni cha lazima katika kikundi fulani cha kirai kinaitwa kichwa. Sifa za kichwa huwa sifa za kirai chote. Kichwa ndicho kipashio muhimu katika kirai kizima. Vipashio vingine si vya lazima.

Nadharia ya X-baa inahusu upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango tofauti katika sentensi. Ni upangaji huu unaobaini ni kipashio kipi kina uhusiano wa ngazi moja na ni kipi kinamiliki kipi. Kwa mfano:

3) *Yule mwanafunzi wa sintaksia mwenye nywele ndefu amepita vyema.*



Radford (1988: 187)

Katika mfano (3) KN kinamiliki kibainishi na N', kibainishi na N' ni cha kiwango kimoja kwa kuwa ni vipashio vinavyomilikiwa na KN. N na KH ni vipashio vya ngazi moja na vinamilikiwa na N'. N' na chagizo ni vipashio vya ngazi moja vinavyomilikiwa na N'. KH ni kijalizo kwa kupanua N hadi N' nacho CH ni chagizo kwa kuwa kinapanua N' hadi N'. Ifahamike kuwa kijalizo, kibainishi na chagizo ni viambajengo huria (si vya lazima). Vinaweza kuwepo au vikaondolewa pasi kuathiri kirai husika. Awali nadharia hii ilitumika kufafanulia virai pekee lakini baadaye kategoria za kiuamilifu kama vile: vishazi, kijalizo, yambwa, kiarifu, vishazi na chagizo zikaingizwa ili kusawazisha muundo wa virai vyote uwe ni muundo ulio na kichwa pekee au unaoandamana na vipashio vingine. Kwa mfano:

4) *Mgeni anaogopa watu sana.*


Muundo wa KN cha (4) chaweza kuchorewa kielelezo tungo kifuatacho:



Wiley na Carnie (1969) wanasema kuwa chagizo hupanua kipashio chochote cha X' hadi X'.Sheria ya chagizo basi itakuwa kama:

$X' \rightarrow X' (ZP)$

Sheria hii itawakilishwa kama ifuatavyo katika kielelezo tungo:




Blackwell na Carnie (1969:338)

Hii inamaanisha kuwa chagizo chaweza kufafanua chagizo kingine kwa sababu sheria ya chagizo ina sifa ya kujirudia inayoonyeshwa na ukweli kuwa katika upande wa kushoto kuna X' na katika upande wa kulia kuna X' pia. Hivyo basi kunaweza kuwa na idadi nyingi ya chagizo katika sentensi fulani. Kwa mfano:

5) Kitabu kile *chenye jalada nyekundu cha mwalimu wetu* kimepotea.

Vipashio *chenye jalada nyekundu na cha mwalimu wetu* ni chagizo za KN *kitabu kile*. Kirai nomino kilicho na chagizo mbili chaweza kuwakilishwa kama ifuatavyo katika kielelezo tungo



Katika mchoro (5) KV na KH ni vipashio vinavyofafanua N' hadi N' jukumu lililo la chagizo.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Sehemu hii ilianguzia kazi za aina mbili: zilizoandikwa kuhusu chagizo na zile zimeandikwa kuhusu nadharia.

### 1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu chagizo

Lyons (1968) anaeleza chagizo kama kipashio cha ufafanuzi kinachofungamanishwa na kichwa cha kirai na kinachokitegemea. Kipashio hiki kinaweza kutolewa bila kuwa na athari yoyote ya kisintaksia ya sentensi husika. Anasema kuwa chagizo zaweza kuwa za kivumishi zinazofafanua nomino ndani ya kirai nomino au za vielezi zinazofafanua kirai tenzi. Anasema kuwa chagizo za sentensi zaweza kuwa za aina nyingi kama vile: virai, vishazi au maneno. Anagawa chagizo kwa makundi tofauti kutegemea uamilifu wake wa kisemantiki katika sentensi. Maelezo haya yalitumika katika utafiti wetu kuonyesha majukumu tofauti ya theta yanayowakilishwa na chagizo zilizo na miundo tofauti katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu.

Carnie (2013) akitumia nadharia ya X-baa, anaelezea chagizo kama kipashio ambacho huchukua kirai cha baa moja na kutengeneza kirai cha baa moja. Anasema kuwa ni kipashio kisicho cha lazima na hakihusiana sana na kirai kinachokifafanua. Anadai kuwa iwapo chagizo itatumiwa pamoja na kijalizo katika sentensi moja, itakuwa mbali na kirai kinachokifafanua. Maelezo haya yalitusaidia kubaini ni vipashio vipi ni chagizo na vipi si chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu ili kuweza kuvichunguza kwa kina kutegemea malengo yetu.

Radford (1988) naye anatoa maelezo ya chagizo kwa kutumia nadharia ya X-baa anaposema kuwa chagizo ni kipashio kinachofafanua kirai cha baa moja hadi kwa kirai cha baa moja cha kategoria fulani. Akiyaelezea mahusiano ya vipashio vinavyounda kirai anatumia istilahi dadake na bintiye

kufafanua chagizo. Anasema kuwa chagizo ni dadake kirai cha baa moja na wakati huohuo bintiye kirai cha baa moja. Maelezo haya yalitufaa katika utafiti huu kwa sababu yalitusaidia kushughulikia muundo wa chagizo kwa kutumia nadharia hii ya X-baa.

Jerono (2003) anaeleza chagizo kama kategoria ambayo hutumika kuelezea vile vipashio vya kuelezea ambavyo mara nyingi huwa vielezi na vihusishi. Maelezo haya yamefungamanisha chagizo na vielezi pekee japo utafiti wetu uliweza kuonyesha kuwa tunaweza kuwa na chagizo ambazo si vielezi. Kazi hii ilitufaa sana katika uchanganuzi wa viambajengo vya chagizo kwa sababu ametumia nadharia ya X-baa kuchanganua miundo ya virai na vishazi arifu ambayo ilitumika kuchanganulia miundo ya chagizo katika utafiti wetu.

Waihiga na Kagwa (2006) wanaeleza chagizo kama vielezi au virai vielezi vinavyotokea katika sentensi au tungo lolote kwa kufafanua kitenzi, kivumishi na kielezi. Ni sehemu ambayo yaweza kutokea au isitokee lakini bado sentensi ikawa na maana kamilifu. Kwa kawaida hutokea baada ya kitenzi japo si lazima kwani chaweza kutokea mahali popote. Tulifaidika kwa maoni haya kwa kuwa yalituwezesha kubaini aina tofauti za chagizo kutegemea aina ya kirai kinachofafanuliwa na chagizo husika.

Matei (2008) alielezea chagizo kama sehemu ya sentensi ambayo huja baada ya kitenzi au yambwa. Alidai kuwa chagizo huwa kielezi, kirai kielezi au kirai kihusishi kinachofanya kazi ya kielezi. Tuliyaona mawazo haya kuwa banifu sana kwa vile yalifunga chagizo kwa kitenzi pekee ilhali utafiti wetu uliweza kuonyesha kuwa kunaweza kuwa na chagizo za virai vinginevyo katika sentensi kama vile chagizo ya kirai nomino au kirai kivumishi.

Mwachanya (2009) anafafanua chagizo kama neno ambalo laweza kujisimamia. Anaongezea kuwa ni kategoria ambayo hutumika kuelezea vipashio vya kielezi ambavyo mara nyingi huwa vielezi au vihusishi. Maelezo haya ni finyu sana kwani kulingana na mtazamo wetu, kipashio chochote cha ziada katika kirai ni chagizo. Alichanganua kishazi kielezi cha Kiswahili.

Koech (2013) anasema kuwa chagizo ni kipashio cha ziada na ambacho kikitolewa hakiathiri maana kusudiwa ya sentensi. Anasema kuwa chagizo hutoa taarifa kuhusu kiarifa. Alielezea kuwa

chagizo na kijalizo ni vipashio vinavyofanana sana kimuundo japo vinatofautiana kwa kuwa chagizo ni kipashio kisichokuwa cha lazima ilhali kijalizo ni kipashio cha lazima. Japo kazi yake ilishughulikia vijalizo kwa kutumia nadharia ya X-baa, ilitusaidia kuelewa tofauti ya kijalizo na chagizo katika sentensi za Kiswahili sanifu. Pia kazi yake ilitusaidia kuchanganua chagizo kwa kutumia nadharia ya X-baa kwa kuwa chagizo na kijalizo ni vipashio vinavyofanana kimuundo tofauti ikiwa kijalizo ni cha lazima ilhali chagizo si cha lazima.

Kuiper na wengine (2014) wanasema kuwa chagizo ni kipashio cha ziada. Akilinganisha sentensi na kiunzi cha mifupa, anasema kuwa chagizo huongezwa kwa kiunzi hiki kwa kutumia kifundo mahali ambapo chagizo yafaa kupachikwa. Kiunzi hiki cha mifupa huundwa na kichwa cha kirai husika (vikiwemo vishazi huru na vishazi vitegemezi) ambacho kirai sharti kiwe nacho. Kila chagizo hufafanua dadake na kuwa chagizo ni kipashio kinachoweza kufafanua kirai chochote. Maelezo haya yalitutolea mwanga kuhusu chagizo hasa zinazotumia vishazi. Pia kazi yake ilihusisha chagizo na majukumu ya kisemantiki ambayo tumeyashughulikia.

Obuchi na Mukhwana (2015) wanaeleza chagizo kama neno au kundi la maneno linalojaza nafasi ya kielezi au vielezi katika tungo au sentensi. Huweza kutokea tu baada ya kitenzi au shamirisho iwapo itatoa sifa zaidi za kitenzi. Chagizo ni kiambajengo cha kikazi kinachotoa taarifa kuhusu kiarifa kwa kutaja jinsi tendo lilifanyika, lini tendo lilifanyika na wapi lilifanyikia. Mawazo haya ya chagizo yana mtazamo tofauti na wa utafiti huu. Pia wameshughulikia virai na vishazi kwa kina na walitufaa kubaini miundo ya chagizo.

Olali (1997) aliangalia kikundi nomino cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya x-bar. Ingawa ilikuwa tofauti na kazi yetu ilitusaidia kuelewa vyema nadharia ya X-baa tuliyoitumia kuchanganulia miundo ya chagizo. Pia alitupa mwanga kuhusu miundo tofauti ya virai nomino. Vile vile alitusaidia kwa kutupa istilahi za nadharia hii katika lugha ya Kiswahili.

Kamau (2002) alilinganisha virai vya Kiswahili sanifu na vile vya Kikuyu cha Kabete kwa kutumia nadharia ya X-baa. Kazi yake ilikuwa mchango mkubwa kwa kazi yetu kwa kutufafanulia miundo tofauti ya kirai.

Mwalili (2008) alitusaidia kwa mawazo yake hasa kuhusu vishazi alipoangazia kishazi nomino cha Kiswahili sanifu. Japo alitumia nadharia tofauti na tuliyoitumia, uainishaji wake wa vishazi vitegemezi ulikuwa mchango mkubwa kwa kazi yetu.

Culicover (2013) alitufaa kwa kutuchochea tuchunguze uhusiano uliopo katika muundo wa chagizo na jukumu la theta linalowakilishwa nacho. Kulingana naye vipashio vya kimuundo vya sentensi fulani huchangia kwa maana itakayowakilishwa na kipashio hiki katika sentensi.

Haegeman (1994) akielezea kuhusu nadharia ya X-baa anashughulikia uchanganuzi wa virai kwa kuzingatia kategoria na uamilifu. Alitufunulia mengi tuliyoyatumia kuchanganulia chagizo ya Kiswahili sanifu.

### **1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Theta**

Blackwell na Carnie (1969) wanadai kuwa sentensi ina vidhibiti vya kisemantiki vinavyojitokeza katika mahali maalum. Njia ya kuviondoa vidhibiti hivi ni kwa kutumia mahusiano ya kisemantiki yanayoonyesha uamilifu wa agumenti katika tungo hasa kuhusiana na vitenzi. Wanasema kuwa majukumu ya theta ndiyo hupatia motisha uhamishaji wa vipashio kwa kuwa kipashio chochote kile hupokea jukumu la theta katika nafasi maalum. Ikiwa kipashio hakimo katika nafasi hii sharti kibandilishiwe nafasi ili kiweze kupokea majukumu ya theta. Maelezo haya yalikuwa muhimu kwa kazi yetu kwa kuwa lengo moja la kazi hii lilikuwa kubaini iwapo chagizo husalia na jukumu lile lile la theta hata baada ya nafasi yake kubadilishwa au huwakilisha jukumu tofauti la theta. Pia yalitusaidia kubaini vipashio vinavyotoa majukumu ya theta kwa vipashio vingine.

Gruber (1970) anasema kuwa sintaksia haifai kuangaliwa kama mfumo wa kaida tu bila kuhusisha semantiki. Anadai kuwa taratibu kadhaa katika sentensi zina umuhimu wa kisintaksia na pia wa kisemantiki. Alishughulikia namna aina za vitenzi hutoa majukumu tofauti ya theta kwa vipashio vya kisintaksia kama vile virai vihusishi. Maelezo haya yalituwezesha kubaini uhusiano uliopo kati ya vipashio leksika na majukumu ya theta yanayotolewa na vipashio vinavyotoa jukumu la theta kwa vipashio hivi.

Anderson (1971) anafafanua uamilifu wa kisintaksia wa vipashio tofauti katika sentensi na jinsi majukumu ya theta hutolewa katika tungo kwa vipashio hivi tofauti. Anaongezea kuwa kitenzi

huchaguliwa mahususi ili kiweze kubaini majukumu tofauti ya theta yanayotolewa kwa agumenti tofauti. Mawazo haya yalitusaidia kufananua uamilifu wa chagizo unaotolewa na vitenzi tofauti kwa kipashio hiki. Hata hivyo ilibainika kuwa vitenzi ambavyo si elekezi ndivyo hufafanuliwa na kipashio chagizo kilicho huria na chagizo hiki hutumika kuwakilisha majukumu tofauti ya theta yanayotolewa kwacho na kitenzi licha ya kuwa kitenzi hakichagui chagizo hizi.

Radford (1988) anasema kuwa kategoria za kileksika zinafaa kuwa na ujumbe kuhusu majukumu ya theta ili kuongezea kwa habari za kategoria na zile za uteuzi. Anaongezea kuwa majukumu ya theta yanaweza kutumiwa kuonyesha kufanana au kutofautiana kwa vipashio fulani ambavyo si dhahiri kupitia kwa miundo ya vipashio hivi pekee. Maelezo haya yalitusaidia kutathmini majukumu tofauti ya kipashio chagizo kilicho na muundo sawia hasa kipashio hiki kinapotokea katika nafasi tofauti katika sentensi.

Cook (1989) akiyarejelea maelezo ya Fillmore (1968) anasema kuwa kuna seti bia za mahusiano dhamirifu yanayoonyesha jukumu muhimu la theta. Mahusiano haya huelezea uhusiano uliopo kati ya sintaksia na semantiki na yanaweza kutumika katika lugha zote. Maelezo haya yalitufaa sana kwa sababu tuliyatumia kupima ubia wa nadharia ya theta kwa kutumia lugha ya Kiswahili kuchanganulia chagizo.

### **1.7.3 Yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya X-baa**

Radford (1988) anasema kuwa nadharia ya X-baa hutumia mfumo wa nambari alizoziita nambari zilizoinuliwa ili kuweka wazi virai vinavyaongezwa kwenye kirai chochote kile. Anasema kuwa kuna mvurumisho wa virai kutoka kwa kategoria za kileksika. Haya maelezo ni muhimu kwani yalitusaidia kutambua miundo tofauti ya chagizo katika sentensi au kirai husika.



Cowper (1992) akizungumzia jinsi kirai kinavyochanganuliwa kimuundo kwa kutumia nadharia hii ya X-baa anaeleza kuwa kina kiambajengo cha kati anachokiita X' kinachoweza kutokea zaidi ya mara moja. Maelezo haya yalitusaidia kubainisha muundo wa chagizo pamoja na viambajengo vyake.

Blackwell na Carnie (1969) wanasema kuwa katika X-baa kipashio cha lazima ni kichwa cha kirai husika. Maneno mengine yote yanayoambatana na kirai husika ni ya ziada. Anapendekeza sheria tatu za kufuatwa inayoonyesha kirai ni cha aina gani, inayochukua kiwango cha baa moja na inayoonyesha kichwa cha kirai husika. Mawazo haya yalitufaa kwa kuwa tuliyatumia kuchanganulia muundo wa chagizo.

Kuiper na wengine (2014) wanasema kuwa katika nadharia ya X-baa, chagizo zote hufafanua vipashio vingine katika sentensi kwa kutoa maelezo ya ziada kuvihusu. Wanaongezea kuwa maelezo haya hupanua kirai cha baa moja hadi kwa kirai cha baa moja. Ni mawazo tuliyoyatumia ili kuweza kubainisha ni vipashio vipi vya kiufafanuzi ni chagizo na ni vipi si chagizo.

Jackendoff (1977) anasema kuwa neno kuu katika kirai chochote kinajulikana kama kichwa cha kirai hicho au X. Kirai kinachobeba X ni X' na kinachobeba X' ni X". Anaongezea kuwa kanuni ya X-baa haikuwezesha X' ipanue X' ambayo ni kanuni inayohusishwa na chagizo. Mawazo haya yanapingana na yetu kwa kuwa msimamo wetu ni kwamba nadharia ya X-baa inaweza kutumika kuchanganulia chagizo kipashio kinachopanua X' hadi X'.

## **1.8 MBINU ZA UTAFITI**

Katika sehemu hii tuliangazia: ukusanyaji wa data, uteuzi wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data pamoja na maelezo ya mbeko za utafiti zilizofuatwa. Uteuzi wa data iliyotumika ulifanywa kimaksudi.

### **1.8.1 UKUSANYAJI WA DATA**

Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa kudondoa sentensi zenye chagizo kutoka kwa vitabu vya Kiswahili ambavyo ni: Matei (2008) *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi kamili wa Sarufi*, Waititu na Ipara (2005) *Kiswahili Fasaha* kidato cha nne na Wamitila (2004) *Chemichemi za Kiswahili*

kidato cha tatu na cha nne. Vitabu hivi vimeandikwa kwa Kiswahili sanifu ambayo ni lugha iliyotumiwa katika utafiti huu. Sentensi zilizodondolewa ziliwekwa kwenye makundi yaliyoonyesha aina ya chagizo zinazopatikana kwenye virai na vishazi tofauti.

Pia tulisoma kazi zilizoandikwa kuhusu nadharia tulizotumia ili kuweza kuzifahamu kwa ukamilifu na kusoma kazi zilizoandika kuhusu chagizo ili kuelewa maana ya chagizo, muundo wa chagizo na majukumu ya theta ya chagizo katika sentensi.

### **1.8.2 UCHANGANUZI WA DATA**

Sentensi zilizodondolewa kutoka kwenye vitabu zilichanganuliwa ili kubainisha chagizo zenye miundo tofauti katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu kisha vipashio mbalimbali vya chagizo vilivyo na miundo tofauti katika sentensi viliweza kuchunguzwa ili kubaini majukumu ya theta ya chagizo mbalimbali. Nadharia ya theta ilitumika kubaini vipashio vilivyotumika katika utoaji wa majukumu hayo ya theta.

### **1.8.3 UWASILISHAJI WA DATA**

Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuonyesha namna chagizo tofauti zinaweza kupokea majukumu ya theta katika virai na vishazi katika Kiswahili sanifu. Aidha vielelezo tungo vilitumika kuonyesha miundo na viambajengo vya chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu. Katika uwasilishaji wa data, kazi hii imeweza kuzingatia utambulishaji na vyanzo vya data iliyotumika.

## **1.9 HITIMISHO**

Katika sura hii, tumewekea msingi mada husika kwa kubainisha kuwa nadharia ya X-baa inaweza kutumika kuchanganulia muundo wa chagizo kwa kukipanua kirai cha aina fulani hadi kwa kirai cha aina hiyo hiyo. Pia ilikuwa wazi kuwa kipashio chagizo kinaweza kuwakilisha majukumu tofauti ya theta katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu. Chagizo ambazo ziliwakilisha majukumu haya tofauti ya theta ni zile zilizokuwa na muundo wa kirai kielezi na kirai kihusishi na majukumu haya yalitolewa kwacho na kitenzi au kihusishi

## **SURA YA PILI**

### **SENTENSI NA VIPASHIO VYAKE**

#### **2.0 UTANGULIZI**

Katika sura ya kwanza tulibaini tatizo letu la utafiti na kuonyesha mbinu za utafiti zitakazotumiwa katika utafiti huu. Tulielezea nadharia za kuchanganulia chagizo cha Kiswahili sanifu zilizokuwa nadharia ya Theta na nadharia ya X-baa. Sura hii itashughulikia sentensi, virai, vishazi na kategoria amilifu za maneno. Hivi ni vipashio tutakavyotumia kuchanganulia chagizo kwa kuonyesha viambajengo vinavyokiunda.

#### **2.1 DHANA YA SENTENSI**

Sentensi ndicho kipashio kikubwa kabisa cha kimuundo chenye maana kamili. Sentensi ni kundi la maneno lililo na kiima na kiarifu. Muundo wa sentensi huhusisha vipashio vingine vidogo kimuundo kama vile virai na vishazi. TUKI (1990) wanasema kuwa kirai ni kipashio cha kimuundo kilicho na zaidi ya neno moja lakini hakina muundo wa kiima kiarifu. Lyons (1968) anaeleza dhana ya kishazi kama kundi la maneno lililo na kiima na kiarifu aghalabu likiwa ndani ya sentensi.

Wamitila (2010:198) anaainisha sentensi katika makundi mawili muundo na kikazi/kiuamilifu. Akielezea anasema kuwa kimuundo sentensi huundwa kwa kikundi nomino na kikundi tenzi na kuwa sentensi kiuamilifu hujihusisha na kiima na kiarifu. Kiima ni sehemu inayozungumziwa na kiarifu ni sehemu inayozungumzia kiima. Kiarifu huambatana na sehemu nyinginezo kama vile: yambwa, kijalizo na chagizo. Kuna aina tatu za sentensi kutegemea muundo ambazo ni: sahili, ambatano na changamano.

Sentensi sahili ni sentensi zinazohusu muundo wa kikundi nomino na kikundi tenzi na wenye maana kamili (Massamba na wengine 2012:153). Sifa kuu ya sentensi hii ni kuwa na taarifa moja iliyo katika kikundi kitenzi. Sentensi hizi hata zikipanuliwa kwa virai vinginevyo, taarifa kuu husalia ile ile.

Sentensi ambatano ni sentensi iliyo na vishazi viwili huru au zaidi vilivyounganishwa kwa viunganishi. Iwapo vishazi hivi vitaondolewa kutoka kwa muundo wa sentensi ambatani, kila kishazi hujitegemea kama sentensi. Sentensi changamano ni sentensi iliyo na kishazi kimoja huru na kingine kitegemezi. Kwa mfano:

- 6) a) *Mama anapika wali vizuri.*
- b) *Mama anapika wali vizuri na baba anaosha gari.*
- c) *Mtoto anayelia sana ameadhibiwa vibaya.*

Sentensi (a), (b) na (c) ni sentensi sahili, ambatano na changamano mtawalia. Sentensi (a) ina maana kamili na imeundwa kwa kikundi nomino *mama* na kikundi kitenzi *anapika wali vizuri*. Nayo (b) ina vishazi viwili huru ambavyo ni: *mama anapika wali vizuri, baba anaosha gari*. Sentensi (c) imeundwa kwa kishazi kitegemezi *mtoto anayelia sana* na kishazi huru *ameadhibiwa vibaya*.

Kigezo cha dhamira huwa na sentensi ya taarifa, sentensi ya masharti, sentensi agizi, sentensi ulizi na sentensi ombi. Sentensi ya taarifa ni sentensi inayojua kuhusu kinachotendwa na kiima. Sentensi ya masharti huonyesha kuwa kuna kitendo kinachotegemea kingine ili kitendeke. Sentensi ulizi ni sentensi zinazohoji kuhusu tendo fulani. Sentensi ombi ni sentensi inayoleta dhana ya kutaka kusaidia au kuomba usaidizi. Kwa mfano :

- 7) a) *Mtoto anaandika barua.*
- b) *Nikimwona nitakujuza.*
- c) *Umekunywa chai?*
- d) *Tafadhali nitilie maji ninywe.*

Sentensi (a), (b), (c) na (d) ni sentensi ya taarifa sentensi ya masharti, sentensi ulizi na sentensi ombi mtawalia.

Sentensi za Kiswahili aghalabu huwa na sehemu mbili kuu ambazo ni kikundi nomino na kikundi kitenzi. Kikundi nomino huundwa kwa nomino pamoja na maneno mengine yanayotumika pamoja na nomino hii na kikundi kitenzi huundwa kwa kitenzi pamoja na maneno mengine yanayoweza kutumika pamoja na kitenzi hiki. Maneno yanayoandamana na vikundi hivi viwili yanaweza kuunda virai. Virai hivi vyaweza kuwa kirai nomino, kirai kitenzi, kirai kivumishi, kirai kihusihi na kirai kielezi.

### 2.1.1 VIRAI

Matei (2008:190) anaeleza kirai kama fungu la maneno linalofanya kazi kama neno moja na huwa na uamilifu sawa na neno hilo. Kwa upande Massamba (2004:35) anaelezea kirai kama kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini hakina uhusiano wa kiima-kiarifu (yaani hakihusishi mtendaji wa tendo na tendo lililotendwa). Nasi tunachukulia kirai kama fungu la maneno linalofanya kazi kama neno moja na hupatikana katika sentensi fulani. Radford (2004:14) anadai kuwa kila kirai kina kichwa ambacho huamua sifa za kirai kizima. Kwa mfano:

8) *Mwanafunzi wa sintaksia ameamua kusoma kwa bidii.*

Kirai *mwanafunzi wa sintaksia* ni kirai ambacho kina neno mwanafunzi kama kichwa cha kirai hiki. Neno hili ndilo litakaloamua sifa za kirai kizima. Aina ya kirai fulani hutegemea neno kuu au kichwa cha kirai hiki. Kwa mfano; Kirai ambacho neno lake kuu ni nomino au kiwakilishi cha nomino kitaitwa kirai nomino. Kwa kutumia mkabala huu kuna aina tofauti za virai ambavyo ni: virai nomino, virai vivumishi, virai vielezi, virai vihusishi na virai vitenzi.

#### 2.1.1.1 Kirai nomino (KN)

Hiki ni kirai kinachofanya kazi kama nomino. Neno kuu la kirai hiki ni nomino au kiwakilishi cha nomino. Nomino ni neno linalotumiwa kutaja mtu, kitu, hali au jambo fulani ilhali kiwakilishi ni neno linalotumika badala ya nomino katika sentensi. Muundo wa kirai nomino umejikita kwa mahusiano yaliyopo kati ya nomino na neno au mafungu mengine ya maneno. Kirai nomino chaweza kuwa kiima, yambwa, kijalizo au chagizo katika sentensi fulani. Kwa mfano:

9) *Mwalimu yule aliadhibu mwanafunzi wake.*

*Mwalimu yule* ni kiima ilhali *mwanafunzi wake* ni yambwa tendwa ambayo ni chagizo.

10) *Yeye mwenyewe aliweka mzigo huu ndani ya kabati lile.*

*Kabati lile* ni kirai nomino kinachoonyesha mahali hivyo basi ni chagizo katika sentensi hii.

Virai nomino katika Kiswahili vyaweza kuwa na miundo ifuatayo:

Nomino pekee yake (N) au kiwakilishi pekee(W):

11) a) *Dada* ameondoka.

b) *Yule* ni mamake.

Nomino mbili zilizounganishwa na kiunganishi (N+U+N) au viwakilishi viwili vilivyounganishwa na kiunganishi( W+U+W):

12) a) *Baba na mama* wanaenda sokoni

b) *Hiki na kile* ni vyao.

Nomino na kivumishi kimoja au zaidi (N+V) au kiwakilishi na kivumishi kimoja au viwili (W+V+V) :

13) a) *Mti mkubwa* umeanguka.

b) *Yule mdogo mchafu* ameokolewa.

Nomino na kishazi kitegemezi (N+S) au kiwakilishi na kishazi (W+S):

14) a) *Mtoto aliyemletea mama kuni* ni mtiifu

b) *Kile kilichopotea jana* kimepatikana leo

Nomino na kirai kihusishi (N+ KH) au Kiwakilishi na kirai kihusishi (W+KH):

15) a) *Tunda la mtoto* limeiva sana

b) *Yule wa mwalimu wetu* amepewa ufadhili kutoka ng'ambo.

### **2.1.1.2 Kirai kivumishi (KV)**

Hiki ni kirai ambacho neno lake kuu ni kivumishi. Kivumishi ni neno linalotoa habari zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi. Aghalabu muundo wa kirai kivumishi huwa wa kivumishi na neno au fungu la maneno linaloandamana na kivumishi hiki. Kirai hiki hutumiwa katika sentensi kufafanulia nomino au kiwakilishi hivyo basi hutumika kama kivumishi katika sentensi husika. Kirai kivumishi hujikita ndani ya kirai nomino japo kinaweza kupatikana kwa kirai kitenzi kinapotumiwa kukamilisha kitenzi kishirikishi. Hata hivyo muundo wa kirai kivumishi ni muundo unaobainika. Kirai hiki chaweza kuwa na miundo ifuatayo:

Kivumishi na kielezi (V+E) :

16) *Mtoto huyo* ni *mtukutu sana*

Kivumishi na kirai nomino (V+KN) :

17) *Mzee yule* ndiye *mwenye duka kubwa*

Kivumishi na kivumishi (V+V) :

18) *Wasichana waliofika walikuwa wengi wafupi.*

Kivumishi na kirai kihusishi (V+KH) :

19) *Ukuta utakaojengwa* ni *huo wa nyumba yangu*

Kivumishi pekee (V) :

20) *Kikombe hiki* ni *safi*

### **2.1.1.3 Kirai kielezi (KE)**

Hiki ni kirai ambacho neno lake kuu ni kielezi. Kielezi ni neno linalotoa maelezo ya ziada kuhusu kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Huundwa kwa mahusiano kati ya vielezi na maneno mengine katika sentensi kama vile: vielezi vingine, vivumishi na vitenzi. Massamba na wengine (2012:116) virai vielezi kujikita kwenye mahusiano yasiyo ya lazima baina ya neno kuu (kielezi) na neno au fungu la maneno linaloandamana nalo. Aghalabu hujitokeza baada ya kitenzi na huchukuliwa kama chagizo. Virai vielezi huwakilisha nafasi ya chagizo kwa kuwa si lazima virai hivi viwepo katika sentensi ili maana ya sentensi husika ibainike. Kirai kielezi chaweza kuwa na miundo ifuatayo:

Kielezi kimoja ( E):

21) *Nyumbani mwake mna watu wengi sasa.*

Vielezi viwili au zaidi ( E+E):

22) *Atakuwa nyumbani kesho*

Kishazi kielezi ( KJ):

23) *Aliadhibiwa ilivyostahili na mwalimu.*

Kielezi na kirai kihusish ( E + KH):

24) *Atafika nyumbani baada ya saa tatu.*

Virai vielezi vyaweza kuwa vya aina nne tofauti vya virai. Aina hizi ni:

Vielezi vya wakati:

25) *Atafika kesho kutwa*

Vielezi vya mahali:

26) *Anafagia nyumbani*

Vielezi vya namna:

27) *Alifagia vibaya*

Vielezi vya idadi:

28) *Atafagia mara tatu*

### **2.1.1.4 Kirai kihusishi (KH)**

Ni kirai ambacho neno lake kuu ni kihusishi. Kihusishi ni neno au fungu la maneno linaloonyesha uhusiano baina ya kitu na kingine au mtu na mwingine. Uhusiano huwa waweza kuwa wa mahali, wakati, kiwango au mtenda. Kirai kihusishi aghalabu huundwa kwa kihusishi na maneno mengine kama vile nomino na kielezi. Kinaweza kutokea mahali popote pale katika sentensi kama vile mwanzoni au mwishoni mwa sentensi. Kirai hiki hutekeleza majukumu yafuatayo ya kisarufi:

Kufafanua nomino kama Kivumishi:

29) Maji ya *mfereji* huu hayanyweki.

Kufafanua kitenzi kama kielezi:

30) Tutakutana *nje ya lango lile kwa muda mfupi*.

Kuwakilishi nomino kama kiwakilishi:

31) *La mama* litaliwa na mwanawe.

Kirai kihusishi katika Kiswahili sanifu chaweza kuwa na miundo ifuatayo:

Kihusishi na nomino(H+N):

32) *Shinikizo la marika* ni tishio kwa nidhamu ya *vijana*.

Kihusishi na kielezi(H+ E ):

33) *Tulimsubiri hadi asubuhi*.

Kihusishi na kishazi ( H+ KJ):

34) *Tulitembea mpaka alipokuwa amesimama*.

#### **2.1.1.5 Kirai kitenzi (KT)**

Hiki ni kikundi cha maneno kinachofanya kazi kama kitenzi. Neno kuu la kirai kitenzi ni kitenzi. Kitenzi ni neno linalotuarifu kuhusu jambo linalotendewa nomino au linalotendwa na nomino. Kulingana na Habwe na Karanja (2004) kitenzi ni neno linaloeleza jambo linalofanywa au linalofanyika. Obuchi na Mukhwana (2015) wanaelezea aina tano za vitenzi. Aina hizi ni vitenzi vishirikishi, vitenzi halisi, vitenzi visaidizi, vitenzi elekezi na vitenzi visoelekezi.

Vitenzi vishirikishi

Vitenzi vinavyoonyesha tabia au hali fulani kwa namna inayoonyesha umoja wa mambo fulani.

Huashiria sifa au vyeo vya wahusika. Kwa mfano:

35) *Ayub ni mwalimu*

Vitenzi halisi

Huelezea kutendeka au kutotendeka kwa jambo ambapo maelezo kuhusu jambo linalofanywa au lisilofanywa yanatolewa. Kwa mfano:

36) *Wanafunzi walitutembelea jana*.

Vitenzi visaidizi

Vitenzi vinavyosaidia vitenzi vikuu kupitisha taarifa fulani. Kwa mfano:

37) *Hamisi huenda akakuoa*.

Vitenzi elekezi



Hivi ni vitenzi vya kutenda vinavyochukua yambwa.kwa mfano:

38) Juma *anacheza* mpira.

Vitenzi visoelekezi

Ni vitenzi visivyochukua yambwa kwa kuwa vimekamilika kimaana. Kwa mfano:

39) Mtoto *analia*.

Kirai kitenzi hujikita kwa mahusiano kati ya kitenzi na maneno mengine. Virai vitenzi vya Kiswahili vina miundo mingi tofauti. Baadhi ya miundo ya kirai kitenzi ni:

Kitenzi pekee( T):

40) *Utapiywa*

Kitenzi na nomino(T +N):

41) *Tumesomewa barua*

Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu (Ts+T):

42) *Alikuwa akitutembelea*

Kitenzi na kielezi(T +E):

43) *Ameingia nyumbani*

Kitenzi na kirai kihusishi(T +KH):

44) *Amepanda juu ya mti*

Kitenzi na kishazi kitegemezi(T+S):

45) *Alifagia alipoonyeshwa.*

Kirai kitenzi na kirai kihusishi(KT+ KH) :

46) *Aliosha sufuria kwa sabuni.*

Kitenzi kishirikishi na nomino(t +N) :

47) *Yeye ni mtoto*

Kirai huwa ni fungu la maneno linalofanya kazi kama aina hii ya neno kama tulivyokwisha taja. Fungu hili halina muundo wa kiima–kiarifu ambao ni muundo unaohusishwa na kishazi katika sentensi.

### **2.1.2 VISHAZI**

Kishazi ni kundi la maneno lenye kiima kimoja na kiarifu kimoja. Kiima ni sehemu ya sentensi iliyo na nomino au kiwakilishi cha nomino pamoja na maneno mengine. Kiarifu nayo ni sehemu ya sentensi inayotoa taarifa kuhusu kiima. Huwa na kitenzi na pengine maneno mengine

yanayoandamana na kitenzi. Aghalabu huonyesha kinachofanyika kwa nomino. Kishazi kinaweza kuainishwa kwa kutegemea muundo wake au uamilifu wake katika sentensi. Vishazi vinavyoainishwa kutegemea muundo ni vya aina mbili: kishazi huru na kishazi kitegemezi. Kishazi huru ni kishazi kinachojitegemea kama sentensi kinapoondolewa kwenye sentensi ambamo kimejikita na kishazi kitegemezi ni kishazi kisichoweza kujitegemea kama sentensi ikiwa kitaondolewa kwenye sentensi kilichomo. Kishazi hiki hutegemea kishazi kingine ili kitoe maana kamili katika sentensi.

### **2.1.2.1 Kishazi huru**

Kishazi huru huwa na vitenzi ambavyo vinaelezea maana kikamilifu. Vishazi hivi havihitaji vishazi vingine ili maana yake ieleweke. Vishazi hivi vikiandamana na vishazi ambavyo haviwezi kujitegemea kama sentensi huitwa vishazi vikuu. Kwa mfano:

48) *Mwanafunzi* aliyesoma kwa bidii *alipita mthani wake*. Sehemu iliyo katika italiki ni kishazi huru

Kishazi hiki hata kikiondolewa katika sentensi kitakuwa na maana na kinaweza kujisimamia kama sentensi. Kishazi huru kinapotolewa kutoka kwa sentensi husika kinaweza kuwa sentensi sahili kikiwa peke yake.

### **2.1.2.2 Kishazi kitegemezi**

Hili ni kundi la maneno ambalo lina kiima na kiarifu hata hivyo haliwezi likasimama peke yake kama sentensi. Vishazi vitegemezi hutegemea vishazi vingine vinavyohusishwa navyo katika sentensi ili vivisaidie kupata maana kamili. Vishazi hivi haviwezi kukubalika kama sentensi kamili ikiwa vitaondolewa kutoka kwa sentensi husika. Vishazi vitegemezi vinaweza kuainishwa ifuatavyo kwa kutegemea uamilifu wake katika sentensi:

Vishazi vitegemezi virejeshi

Hiki ni kishazi ambacho hufanya kazi kama kivumishi. Vishazi huundwa kwa ‘amba’ au ‘o’ rejeshi. Ni vishazi vinavyoturejeshi nyuma kwa jambo ambalo tayari lishazungumziwa. Hupatikana kwenye kirai nomino au hata kirai kitenzi. Kwa mfano:

49) *Jino lililong’olewa jana lingali linaniuma.*

Vishazi vitegemezi vya masharti

Vishazi hivi vitegemezi huundwa kwa viambishi -ki,- nge,- ngali na -po. Pia vishazi hivi vinaweza kuundwa kwa viunganishi vya masharti kama vile: ikiwa.endapo, iwapo. Kwa mfano

50) a) *Ningempa ushauri angeacha tabia mbaya.*

b) *Ikiwa nitamwona Juma nitamsalimia.*

Vishazi vitegemezi vya sababu

Huelezea ni kwa nini kitendo kimefanyika. Vishazi hivi huundwa kwa viunganishi vya sababu au vihusishi vya sababu. Kwa mfano:

51) *Kwa sababu ya kujiuzulu kwa kasisi huyo, utaratibu wa ibada ulibadilishwa.*

Vishazi vitegemezi vya kinyume

Hivi ni vishazi vinavyoundwa kwa viunganishi ambavyo huonyesha kinyume cha mambo au hali ya ukinzani katika kitenzi. Huundwa kwa maneno kama vile: japo.icha ya, ingawa. Kwa mfano:

52) *Ingawa mama huyo aliwapenda watoto wake, hakuwadekeza kamwe.*

Vishazi vitegemezi vya wakati

Hivi ni vishazi vinavyotumiwa kutambulisha wakati katika sentensi. Hutumia vihusishi au viunganishi vya wakati. Hujibu swali lini? Maneno kama vile tangu, baada ya, kabla ya pamoja na kiambishi po yaweza kutumika kuundia vishazi vya aina hii. Kwa mfano:

53) a) *Baada ya gari hilo kuanza safari aligundua alikuwa amesahau mzigo wake ndani.*

b) *Mama alipoiona hali yangu alianza kulia.*

Vishazi vitegemezi vya mahali

Hivi ni vishazi vitegemezi vinavyoonyesha mahali ambapo tendo litatendeka. Hubainika kwa matumizi ya vihusishi au viunganishi vya mahali kama vile mpaka, hadi na viambishi vinavyoonyesha mahali ambavyo ni -po, -ko, -mo. Hujibu swali wapi? Kwa mfano:

54) *Jubi alimuuliza mwanafunzi huyo alikoishi mwalimu Saumu.*

Vishazi vitegemezi vinavyoonyesha matokeo

Hivi ni vishazi vitegemezi vinavyotambulishwa kwa kuwepo kwa viunganishi vya matokeo pamoja na kiambishi -ka. Hujibu swali kwa matokeo gani? Kwa mfano:

55) *Mama huyu alimtesa mwanawe akashifiwa na wengi.*

Vishazi vitegemezi vya namna au jinsi

Ni vishazi vinavyotumika kuonyesha namna tendo fulani linatendeka au namna kitu au mtu alivyo.

Vishazi hivi huundwa kwa kirejeshi -vyo' - pamoja na neno vile. Kwa mfano:

56) Sipendi vile anavyokula akizungumza.

Vishazi vitegemezi vya kiasi

Hivi ni vishazi vinavyoundwa kwa vihusishi vya kulinganisha kama vile kama, kuliko, zaidi ya na kushinda. Vishazi hivi hufanya kazi ya vielezi vya kiasi katika sentensi. Kwa mfano:

57) Mungu anatupenda zaidi ya tunavyompenda.

Sentensi haijumlishwi kwa virai na vishazi pekee. Kuna uwezekano wa sentensi za Kiswahili sanifu kuwa na vipashio vya kikazi kama vile kiima na kiarifu. Vipashio hivi hujulikana kama kategoria amilifu katika sentensi.

### **2.1.3 KATEGORIA AMILIFU ZA SENTENSI**

Uamilifu ni neno linalotumiwa kuelezea jukumu linalotekelezwa na vipashio tofauti katika sentensi. Maneno yanaweza kutekeleza majukumu ya kisarufi yafuatayo katika sentensi. Majukumu haya ni: kiima, kiarifu, yambwa/shamirisho, kijalizo na chagizo.

#### **2.1.3.1 Kiima**

Hiki ni kipashio katika sentensi kinachohusika na utendaji wa kitendo. Obuchi na Mukhwana (2010:167) wanaelezea kiima kama sehemu ya sentensi inayodokeza kinachozungumziwa katika sentensi. Kiima chaweza kuwa neno moja au kundi la maneno. Kwa mfano:

58) a) *Juma* amefika.

b) *Juma aliyetoka ng'ambo* jana amefika.

*Juma* na *Juma aliyetoka ng'ambo* ni viima vya sentensi (a) na (b) mtawalia.

Massamba (2004:32) anafafanua aina zifuatazo za viima:

Kiima ambatani

Hiki ni kiima kilicho na nomino au viwakilishi viwili:

59) *Mtoto na mama* wanatembea.

Kiima dhahiri

Hiki ni kiima kinachohusika na utendaji wa kitendo kwa njia ya wazi:

60) *Dereva yule* huendesha kwa kasi

Kiima fiche

Huwa ni kiwakilishi cha kiima kinachorejelewa kisicho dhahiri. Kwa mfano:

Kiambishi {a} katika kitenzi *alimchapa* ni kiima fiche.

Kiima mantiki

Hili ni neno ambalo ingawa haliko katika sehemu ya mwanzo ya sentensi,ndilo neno linalowakilisha mtendaji wa tendo katika sentensi. Kwa mfano:

61) Wanafunzi wanafunzwa na *mwalimu mgeni*.

Kiima sarufi

Ni kiima kinachotokea mwanzoni mwa sentensi na huwa ndicho kichwa cha sentensi husika. Kwa mfano:

62) *Kitabu* kinasomeka.

### **2.1.3.2 Kiarifu**

Hii ni sehemu ya sentensi ambayo huarifu kiima. Habwe na Karanja (2004:162) wanaelezea kiarifu kama sehemu ya sentensi ambayo inatoa taarifa kuhusu kiima. Hapa ndipo kitenzi kikuu hujitokeza. Kitenzi huonyesha jambo linalofanywa na kiima. *Kuna* uwezekano wa kiarifu kutoa taarifa zifuatazo kuhusu : Kiima ni nini? Kiima kina nini? Kiima kinafanya nini? au kiima kinahisi nini? Kama ilivyo katika sentensi (a-d) hapa chini:

63) a) *Yeye ni mwalimu*

b) *Mtoto ana nywele*

c) *Juma amekunywa chai*

d) *James ana maumivu*

Kiarifu kinaweza kinaweza kujitokeza pamoja na kiima dhahiri na kiima kisicho dhahiri. Kwa mfano:

64) *Unatoa mwangaza hafifu*

Sentensi (64) inawakilisha kiarifu ambacho kimetokea pamoja na kiima kisicho dhahiri. Mifano iliyotolewa hapo juu inaonyesha kiima kinachotokea pamoja na viima dhahiri. Kiarifu cha sentensi ya Kiswahili sanifu chaweza kutumika pamoja na viambajengo vinginevyo vya kimuundo. Viambajengo hivi vyaweza kuwa kijalizo,chagizo au shamirisho/yambwa.

### **2.1.3.3 Yambwa /shamirisho**

Yambwa ni nomino au kiwakilishi ambacho hupokea kitendo katika sentensi. Hupokea kitendo kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Matei (2008:216) anadai kuwa yambwa hujibu maswali: nini, kwa nani na alitumia nini? Yambwa yaweza kuwa nomino, kirai nomino, kiwakilishi au kiambishi. Kuna aina tatu za yambwa:

Yambwa tendwa(shamirisho kipozi)

Ni nomino ambayo imeelekezewa tendo kwa njia ya moja kwa moja. Kwa mfano:

65) Anachemsha *maji*.

Yambwa tendewa( shamirisho kitondo)

Huwakilisha mtu ambaye anaathiriwa na kitendo kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Huyu ni mtu anayepokea faida au hasara ya kitendo. Kwa mfano:

66) Mama anampikia *mtoto* uji.

Yambwa ala(shamirisho kitumizi)

Hiki ni kifaa ambacho ingawa hakipokei tendo kinafanikisha tendo. Ni kifaa kinachohusika katika utendaji wa tendo. Kwa mfano:

67) Ameandika kwa *wino*.

Yambwa katika sentensi yaweza kutumika kama kijalizo kwa kuwa inaweza kuwa inakamilisha wazo fulani hasa pale imejitokeza pamoja na kitenzi kishirikishi au kitenzi kielekezi

#### **2.1.3.4 Kijalizo**

Hiki ni kipashio kinachotumiwa kukamilisha kipashio kingine katika sentensi. Matei (2008:219) anasema kuwa kijalizo ni neno au kirai ambacho hufuata kitenzi kishirikishi na ambacho huelezea zaidi kuhusu kiima au yambwa. Habwe na Karanja (2012:164) wanadai kuwa kijalizo ni neno ambalo hukamilisha kiarifu ambapo kuna kitenzi kisicho cha uarifishaji mkamilifu. Tunakubaliana na maoni ya Matei (2008) kuwa kijalizo ni kipashio kinachofuata kitenzi kishirikishi. Hata hivyo tunaongezea kuwa ni kipashio chochote kile kinachotumika kufafanua kipashio kingine katika sentensi ambacho ni cha lazima. Kwa mfano:

68) a) Harriet ni *mwerevu*.

b) Mwalimu wa *shule hiyo* amepewa mamlaka.

*Mwerevu na shule hiyo* ni vipashio ambavyo sharti viwepo ili sentensi hizi ziwe kamili kimaana. Matei (2008:219) anaelezea aina mbili za kijalizo:

Kijalizo cha kiima

Ni kipashio kinachokamilisha kiima:

69) Hawa ni *majirani wetu*.

Kijalizo cha yambwa

Ni kipashio kinachokamilisha yambwa:

70) Rais amemchagua Juma *kuwa waziri*.

Kijalizo chaweza kuwa :

Nomino (kiwakilishi) au kirai nomino:

71) Yeye ni *daktari hodari*.

Kivumishi au kirai kivumishi:

72) Juma amekuwa *safi*.

Kielezi au kirai kielezi:

73) Mwalimu yu *darasani*.

Kirai kihusishi:

74) Kiatu kilikuwa *chini ya meza*.

Kishazi kitegemezi:

75) Aliaahidiwa kuwa *angesaidiwa*.

Kijalizo na chagizo aghalabu huwa na muundo unaokaribiana sana japo ni vipashio tofauti. Kijalizo huwa ni kipashio cha lazima ambacho hutoa habari muhimu kuhusu kirai husika ilhali chagizo ni kipashio ambacho si cha lazima ( Radford 1988:175). Anaongezea kuwa pamoja na kijalizo na chagizo, kibainishi pia hutumika kufafanua nomino.

#### **2.1.3.5 Kibainishi**

Kibainishi ni kipashio kinachoonyesha urejeleaji wa nomino hasa kikitumika kabla ya kiima cha sentensi husika. Aghalabu huwa vivumishi vionyeshi vinapotangulia kiima. Kwa mfano:

76) *Yule* mwanafunzi wa Fizikia amefurahi sana. Katika sentensi (76) *yule* ni kibainishi cha KN *mwanafunzi wa Fizikia*.

#### **2.1.3.6 Chagizo**

Chagizo ni kipashio cha ziada (kisichokuwa cha lazima) ambacho kinaweza kutolewa katika sentensi pasi na kuathiri maana inayokusudiwa katika sentensi husika. Waihiga na Kagwa (2006) wanaelezea chagizo kama kielezi au kirai kielezi kinachotokea katika tungo lolote lile. Aghalabu hutokea baada ya kitenzi japo si lazima kwani chaweza kutokea mahali popote au kwenye kirai chochote kile. Kwa mfano:

77) Mtoto ameketi *chini ya mti*.

*Chini ya mti* ni chagizo inayofafanua kitenzi ameketi. Chagizo ni kiambajengo cha kikazi kinachotoa taarifa kuhusu kiarifu.


Chagizo ni kipashio cha kiufafanuzi kinachofungamanishwa na kichwa kinachokitegemea na ambacho kinaweza kutolewa pasi kuwepo na mabadiliko ya kisintaksia ya sentensi husika.

Chagizo katika sentensi chaweza kuwa neno, kirai au kishazi na kinaweza kuwekwa katika makundi tofauti kulingana na majukumu yake ya theta (Lyons 1969:344)

Blackwell na Carnie (1969) wakifafanua chagizo wanasema kuwa chagizo aghalabu huundwa kwa vihusishi kama vile: juu ya, hadi pamoja na vivumishi kama vile –enye. Mawazo haya yametusaikia kubainisha chagizo katika lugha ya Kiswahili kwa kuwa chagizo katika lugha ya Kiswahili huweza kuundwa kwa vihusishi na vivumishi na vilevile huundwa kwa vielezi, vishazi na nomino. Isitoshe vihusishi vinavyotumika kama chagizo katika lugha ya kiswahili aghalabu hufanya kazi kama kielezi. Kwa mfano:

78) Kitabu kile *chenye jalada nyekundu* kimepotea.

KV *chenye jalada jekundu* katika sentensi (78) ni chagizo kwa kuwa kirai hiki kinatoa habari za ziada tu kuhusu kitabu kile. Mchoro wa KN kilicho na chagizo waweza kuwakilishwa ifuatavyo:




Katika kielelezo tungo (78) *chenye jalada nyekundu* ni chagizo inayopapanua N' hadi N' ambalo ni jukumu la chagizo katika nadharia ya X-baa kwa kuwa chagizo hupanua kipashio chochote cha X' hadi X'.

Vipashio ambavyo ni chagizo vinaweza kufafanua vingine vilivyo chagizo kwa kuongeza vipashio ambavyo ni chagizo. Hii ni kwa sababu sheria ya chagizo ina sifa ya kujirudia inayoonyeshwa na



ukweli kuwa katika upande wa kushoto kuna X' na katika upande wa kulia kuna X' pia. Hii yamaanishwa kuwa unaweza kuwa na idadi kubwa ya chagizo katika sentensi fulani. Kwa mfano: 79) Kitabu kile *chenye jalada nyekundu cha mwalimu wetu* kimepotea.

Vipashio *chenye jalada nyekundu na cha mwalimu wetu* ni chagizo za KN *kitabu kile*. Kirai nomino kilicho na chagizo mbili chaweza kuwakilishwa kama ifuatavyo katika tungo:




KV na KH katika kielelezo tungo (79) zote ni chagizo kwa kuwa zote zinapanua N' hadi N'.


Kulingana na Lyons (1968) kunaweza kuwa na chagizo kinachofafanua maneno kama vile kivumishi kinachofafanua nomino ndani ya kirai nomino au kielezi kinachofafanua kitenzi ndani ya kirai kitenzi na chagizo kinachofafanua sentensi kama vile maneno, virai na vishazi. Kwa mfano:

80) Kiatu hicho kizuri kitanunuliwa *kesho*.

Kipashio kilicho katika italiki katika sentensi (80) ni chagizo ya neno *kitanunuliwa*. Chagizo hii yaweza kuwakilishwa ifuatavyo katika kielelezo tungo:



KE *kesho* ni chagizo ya kitenzi *kitanunuliwa* kwa kuwa kinapanua T' hadi T'. Katika sentensi kipashio *hicho kizuri* kinafafanua nomino *kiatu* lakini si chagizo kwani fungu hili linapanua N hadi N'. kipashio hiki ni kijalizo. Chaweza kuwakilishwa ifuatavyo:



Kuna viambajengo vya kategoria tofauti vinavyofanya kazi kama chagizo. Hivi ni vielezi, virai vielezi, virai vihusishi na vishazi vitegemezi. Vipashio hivi hutekeleza jukumu hili la chagizo kwa kuwa hata vikiondolewa katika kirai kilichofungamanishwa nacho, maana ya kirai hiki haiathiriki.

## **2.2 HITIMISHO**

Katika sura hii dhana tofauti tofauti zitakazotumika katika utafiti wetu zimewekwa wazi. Tumefafanua dhana ya sentensi, kirai kama vile: kirai nomino, kirai kivumishi, kirai kielezi, kirai kihusishi na kirai kitenzi. Tumepambanua viambajengo tofauti vya virai hivi. Dhana ya kishazi na aina zake tofauti pia imefafanuliwa. Tulielezea kategoria amilifu za maneno kama vile: yambwa, kijalizo, kiima, kiarifu na chagizo. Tuliweza kubaini kuwa virai na vishazi vya Kiswahili sanifu vimeundwa kwa viambajengo tofauti. Kila kirai kilikuwa na miundo yake tofauti iliyokitambulishwa. Ilikuwa wazi katika utafiti huu kuwa virai na vishazi katika Kiswahili sanifu vilikuwa vina uhusiano na kategoria amilifu za sentensi kama kijalizo, chagizo na yambwa.

Virai na vishazi vilivyokuwa na miundo tofauti vingetumika kuwakilisha kategoria hizi amilifu. Kwa mfano tuliweza kuonyesha kuwa kirai nomino kiliweza kutumika kama kiima, kijalizo au hata chagizo na kuwa chagizo zaweza kuwa na muundo wa KN, KH na KE.

## **SURA YA TATU**

### **AINA YA CHAGIZO NA VIAMBAJENGO VYAKE**

#### **3.0 UTANGULIZI**

Katika sura ya pili, vipashio vya kimsingi katika sentensi kama vile: virai, vishazi, yambwa au shamirisho, kiima, kiarifu, kijalizo na chagizo viliwekwa wazi. Katika sura ya tatu tutalenga kuangazia miundo ya chagizo na aina za chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya X-baa ili kuonyesha viambajengo tofauti vilivyounda chagizo hizi.

#### **3.1 AINA YA CHAGIZO**

Virai vyote vya kileksika vinavyoundwa kwa kategoria kuu za maneno vyaweza kutolewa maelezo ya ziada yasiyo ya lazima. Pia kategoria za kiuamilifu kama vile vishazi vyaweza kufafanuliwa zaidi kwa kutumia vipashio vingine. Hii ina maana kuwa tunaweza kuwa na aina za chagizo za aina kuu za maneno na pia za vishazi. Kufuatia haya, tunaweza kuwa na aina hizi za chagizo:

- a) Chagizo za virai
- b) Chagizo za vishazi

##### **3.1.1 CHAGIZO ZA VIRAI**

Tunaweza kuwa na aina zifuatazo za chagizo za virai:


- a) Chagizo cha kirai nomino
- b) Chagizo cha kirai kitenzi
- c) Chagizo cha kirai kivumishi
- d) Chagizo cha kirai kielezi
- e) Chagizo cha kirai kihusishi

##### **3.1.1.1 CHAGIZO ZA KIRAI NOMINO**

Chagizo cha kirai nomino ni neno au kundi la maneno linalotumika kutoa maelezo ya ziada kuhusu nomino au kiwakilishi chake ndani ya kirai nomino. Radford (1988:196) anasema kuwa kuna makundi matatu yanayotumika kufafanua nomino ambayo ni: kibainishi, kijalizo na chagizo. Hata hivyo katika lugha ya Kiswahili, si lazima kibainishi kipanue N' hadi N" kwa vile N' inaweza kujiinua yenyewe hadi N". kwa mfano:

81) Kiatu *cha mama* kimepotea

KH *cha mama* kimepanua nomino kiatu hadi N' ambayo ni *kiatu cha mama*. Nayo N' inajiinua hadi N'' bila kuwepo kwa kibainishi. Maelezo haya yanadhihirika kwenye kielelezo tungo kifuatacho:




Chagizo za KN zaweza kuwa na miundo ya: kirai kivumishi, kirai kihusishi, kirai kielezi na kishazi kitegemezi.

KH kinaweza kutumika katika sentensi kutoa maelezo ambayo ni ya ziada (si ya lazima) katika kirai nomino. Cowper (1992:25) anasema kuwa nomino ambazo hazina sifa za kielelekezi hutumia chagizo iliyo na muundo wa kirai kihusishi kukitolea maelezo ya ziada. Kwa mfano:

82) Wale wanafunzi warefu *wa shule hii* ni watiifu.

KH *wa shule hii* kinatoa taarifa ya ziada kuhusu *wale wanafunzi warefu* na iwapo kitaondolewa sentensi itakayosalia bila chagizo hii itakuwa sahihi kimuundo na maana yake itaeleweka kikamilifu. Kirai nomino cha sentensi hii kimefafanuliwa na vipashio vingine ambavyo ni kibainishi na kijalizo. *Wale* katika KN hiki ni kibainishi ilhali *warefu* ni kijalizo. Kirai nomino cha sentensi (82) kilicho na chagizo na vipashio vinginevyo kinaweza kuwakilishwa kama ifuatavyo kwenye kielelezo tungo:




KH *wa shule hii* katika kielelezo tungo (82) kinapanua N' hadi N' jukumu ambalo ni la chagizo kwa kutumia nadharia ya X-baa .

Hata hivyo baadhi ya virai vihusishi vinavyotumika kufafanua nomino hutumika kama vijalizo hasa virai vihusishi hivi vikiwa vimetumika pamoja na nomino elekezi. Kwa mfano

83) a) Mwenyekiti *wa chama hicho* amejiuzulu.

b) Mwenyekiti amejiuzulu.

Katika sentensi (83a) msomaji anafahamikiwa ni mwenyekiti wa nini anayezungumziwa pasi kuachwa na maswali yasiyojibiwa (kama vile: mwenyekiti wa? Yupi? Nani? ) kwa kuwepo kwa KH *wa chama hicho* ilhali katika sentensi (83b) msomaji anaachwa akijiuliza maswali haya kwa kuwa mwenyekiti husika hafahamiki vyema. Sehemu hii ya KH sharti iwepo ili sentensi yenyewe iweze kukamilika kimaana kwa sababu nomino mwenyekiti ni nomino elekezi inayohitaji kijalizo ili maana yake ikamilike. Kirai nomino kilicho na kijalizo chaweza kuwakilishwa kama ifuatavyo katika kielelezo tungo hiki:




Katika mchoro (83), KH *wa chama hicho* si chagizo ni kijalizo kwa kuwa kinapanua N hadi N' ambalo ni jukumu la kijalizo si la chagizo kwa kutumia nadharia ya X-baa.

Kirai kivumishi kinaweza kuchukua nafasi ya chagizo ya kirai nomino kwa kutoa maelezo ya ziada kuhusu kirai nomino husika ambayo si ya lazima. Kwa mfano:

84) Mfanyabiashara yule *mwenye duka kubwa* amesafiri sana

KV *mwenye duka kubwa* ni chagizo ambacho kina muundo wa KV na hata kikiondolewa kutoka kwa sentensi hii, sentensi hii bado itawasilisha maana kusudiwa vyema. Kivumishi kionyeshi *yule* kimetoa maelezo kuhusu mfanyabiashara. *Yule* katika kirai hiki ni kijalizo. Kirai nomino kilicho na chagizo kitaweza kuwakilishwa ifuatavyo katika kielelezo tungo:




Katika mchoro (84), KV kinapanua KN kutoka kwa N' hadi kwa N'.

Kishazi kitegemezi kinaweza kutumika kutoa maelezo ya ziada kuhusu kirai nomino hasa ikiwa kishazi kitegemezi hiki ni kipashio kisicho cha lazima kwenye kirai nomino. Ikitokea hivyo, kishazi kitegemezi kitakuwa chagizo kwa kupanua N' hadi N'. Kwa mfano:

85) Yule mtu mfupi *anayelima shamba* ni mkulima.

Kishazi kitegemezi *anayelima shamba* katika sentensi (85) ni chagizo kinachotoa ufafanuzi wa ziada wa kirai nomino *yule mtu mfupi*. Kwa kutumia kivumishi cha sifa *mfupi*, wasifu wa mtu yule umebainika. Kipashio chagizo cha sentensi hii kinatoa maelezo ya ziada tu . mfupi ni kijalizo cha KN hiki. Kirai nomino husika kinaweza kuwakilishwa na kielelezo tungo kifuatacho:



Katika kielelezo tungo (85) kishazi kitegemezi *anayelima shamba* ni chagizo kwa kuwa kimepanua N' hadi N'.

### 3.1.1.2 CHAGIZO CHA KIRAI KITENZI

Kitenzi hakina uwezo wa kuteua chagizo ambayo inaweza kukifafanua kwa kuwa chagizo ni kipashio huria katika sentensi. Kwa hivyo chagizo chochote kile chaweza kutumika kufafanua kitenzi chochote kile (Radford 1988:239). Kwa mfano chagizo cha wakati *kesho asubuhi* kinaweza kutumika kufafanua kitenzi chochote kile. Kwa mfano:

86) Mama ataenda/atatembea/atatabasamu *kesho asubuhi*

Katika sentensi (86) chagizo *kesho asubuhi* inaweza kutumika pamoja na vitenzi vyote vitatu ambavyo ni: *ataenda, atatembea na atatabasamu*. Vitenzi vinavyochukua chagizo aghalabu huwa vitenzi visoelekezi. Hivi ni vitenzi visivyochukua yambwa kwa kuwa vimekamilika kimaana hata bila yambwa. Vitenzi hivi huongezewa chagizo ili vitolewe maelezo ya ziada tu. Kwa mfano:



87) Yohana anafanya kazi *ofisini leo*.

Katika sentensi (87) *ofisini leo* ni chagizo kwa vile hata kikiondolewa katika sentensi hii, sentensi itaeleweka pasi msomaji kutatizika.


Radford (1988) anasema kuwa ni vigumu kuweza kubaini ikiwa kipashio cha ufafanuzi kinachojitokeza baada ya kitenzi ni chagizo au kijalizo kwa sababu kipashio hiki kimoja kinaweza kutumika kama chagizo au kijalizo katika sentensi tofauti. Katika lugha ya Kiswahili, haya hutokea iwapo kipashio fulani kimetumika kufafanua vitenzi vilivyo na sifa za kitenzi elekezi na vile vilivyo na sifa ya kitenzi kisichoelekezi. Vitenzi ambavyo vina sifa ya uelekezi hutolewa maelezo ya ziada na kijalizo ilhali vile vilivyo na sifa ya visoelekezi hutolewa maelezo ya ziada na chagizo.

Kwa mfano:

88) a) Mtu huyo anatembea *kwa miguu*.

b) Mama aliwapikia wanawe *kwa mwiko*.

*Kwa miguu* ni KH kinachoweza kutumika kama chagizo ya kitenzi *anatembea* kwa kuwa kitenzi hiki ni kisichoelekezi ilhali *kwa mwiko* ni kijalizo kinachojaliza kitenzi *aliwapikia* kwa kuwa kitenzi *pika* ni kitenzi kilicho na sifa ya uelekezi (kinaweza kuchukua kijalizo). Kirai kitenzi kilicho na chagizo chaweza kuwakilishwa kama ifuatavyo katika kielelezo tungo:



Katika (88) KH *kwa miguu* ni chagizo kinachopanua T' hadi T'

Radford (1988:234) anatofautisha kijalizo na chagizo kwa kusema kuwa nomino iliyotumika kama kijalizo yaweza kuwa kiima cha sentensi husika ikifanyiwa mageuzi ya kimuundo na kuwa sentensi tendwa. Nomino hii ikitumika kama kiima haivurugi usahihi wa sentensi hiyo lakini nomino iliyo ndani ya KH ambacho ni chagizo ikitumika kama kiima cha sentensi iliyogeuzwa kuwa sentensi tendwa, sentensi iliyofanyiwa mageuzi ya kimuundo haitakuwa sahihi kisarufi. Kwa mfano:

89) a) *Watu wengi hufanya kazi kwa ofisi hii.*

\* b) *Ofisi hii inafanywa kazi na watu wengi.*

Sentensi (89b) si sahihi kisarufi kwa kuwa sentensi hii imetumia nomino *ofisi* iliyo sehemu ya chagizo kama kiima chake baada ya kufanyiwa mageuzi ya kimuundo na kuwa kauli tendwa.

Madai haya ya Radford (1988) huenda yakaweza kupingwa katika lugha ya Kiswahili kwa kuwa nomino iliyo mojawapo ya viambajengo vya chagizo iliyoundwa kwa KH yaweza kutumika kama kiima cha sentensi husika ikifanyiwa mageuzi na kuwa sentensi tendwa. Kwa mfano:

c) *Ofisi hii hufanyiwa kazi na watu wengi.*


Sentensi (89c) inaonyesha kuwa nomino iliyotumika kama chagizo katika (89a) inaweza kuwa kiima cha sentensi tendwa baada ya kufanyiwa mageuzi pasi kuvuruga usahihi wa sentensi husika na kwa hivyo kuyapinga mawazo yaliyotolewa na Radford (1988).

Chagizo za kirai kitenzi zaweza kuwa zimeundwa kwa kielezi, kirai kielezi au kirai kihusishi kinachofanya kazi ya kielezi. Kwa mfano:

90) *Mama ataamka asubuhi sana*

*asubuhi sana* ni chagizo ya KT *ataamka* ambayo imeundwa kwa kirai kielezi *asubuhi sana*.

Yaweza kuwasilishwa kama ifuatavyo katika kielelezo tungo:




KE *asubuhi sana* katika (90) kinapanua T' hadi T' ambalo ni jukumu la chagizo katika sentensi.

Virai vihusishi vilevile vinaweza kutumika kama chagizo ya kitenzi. Virai vihusishi hivi aghalabu hutumika kufanya kazi ya vielezi katika sentensi. Kwa mfano:

91) Mama anatembea *kando ya barabara*.

KH *kando ya barabara* katika (91) ni chagizo ambayo inaweza kuwasilishwa ifuatavyo katika kielelezo tungo ikiwa pamoja na KT inayotumiwa kukifafanua:



KH *kando ya barabara* ni chagizo katika mchoro huu kwa kuwa kinapanua N' hadi N'



Nomino nazo zaweza kutumika kufafanua kitenzi kama chagizo. Nomino hizi zaweza kuwa nomino za pekee au nomino za kawaida zilizongezewa kiambishi –ni ili kuwa vielezi vya mahali. Kwa mfano:

92) a) Ametembea *Kisumu*

b) Juma alilala *kitandani*

*Kisumu* na *kitandani* ni chagizo ambazo zimeundwa kwa nomino katika sentensi (92a) na (92b).

Chagizo hizi zaweza kuwasilishwa ifuatavyo katika vielelezo tungo (a) na (b) mtawalia:




Katika mchoro (a na b), N *Kisumu na kitandani* zinapanua N' hadi N' mtawalia.

Matei (2008:205) anasema kuwa vishazi vitegemezi vinaweza kutumika kama chagizo zinazotambulisha mahali, wakati au namna. Kwa mfano:

93) Walifika walipovificha vitabu

*walipovificha vitabu* ni chagizo kwa kuwa kitenzi *fika* kinaeleweka bila kuwepo kwa sehemu hii inachokifafanua. Chagizo hii inaweza kuwakilishwa ifuatavyo katika kielelezo tungo ikiwa pamoja na kitenzi inachokifafanua:



Kishazi kitegemezi *walipovificha vitabu* katika kielelezo tungo (93) ni chagizo kwani kinainua T' hadi T' jukumu linalotekelezwa na chagizo katika X- baa


### 3.1.1.3 CHAGIZO CHA KIRAI KIVUMISHI

Kulingana na Radford (1988) chagizo cha virai vivumishi aghalabu huwa KH hasa katika lugha ya Kiingereza. Maelezo haya yanatofautiana na maelezo ya chagizo za KV katika lugha ya Kiswahili kwa kuwa chagizo za kirai kivumishi huchukua muundo wa kielezi au kirai kielezi. KH kinapotumika baada ya KV huwa ni ufafanuzi wa ziada wa KN wala si wa KV. Kwa mfano:

94) a) Mhimili huu *wa nyumba yake* umedhoofika


b) Watu wengi *weusi tititi* hutoka Afrika

*wa nyumba yake* katika (a) ni kijalizo cha kivumishi *huu* kilichoundwa kwa KH ilhali *tititi* ni chagizo ya kirai kivumishi iliyoundwa kwa kielezi pekee. Maelezo haya yaweza kuwakilishwa kama ifuatavyo katika kielelezo tungo:



KH *wa nyumba yake* katika kielelezo tungo (94) kimetumika kupanua KV kutoka kwa V hadi V' kwa hivyo ni kijalizo wala si chagizo.

Kirai kielezi au kielezi kinaweza kutumika kufafanua kirai kivumishi kwa kukitolea maelezo ya ziada ya kirai kivumishi husika. Kwa mfano katika sentensi (94b) Chagizo hiki chaweza kuwakilishwa kama ifuatavyo katika kielelezo tungo kinapoandamana na KV kinachokifafanua:



Katika mchoro huu kielezi tititi kinapanua V' hadi kwa V'

### 3.1.1.4 CHAGIZO ZA KIRAI KIHUSISHI


Virai vihusishi vyaweza kufafanuliwa zaidi kwa kuongezewa chagizo (Radford: 1988). Katika lugha ya Kiswahili chagizo za KH zaweza kuundwa kwa KE, KH, KV na KT.

Kielezi au kirai kielezi kinaweza kutumika kutoa maelezo ya ziada kuhusu kirai kihusishi.

kwa mfano:

95) Aliingia kwa masaibu *kabisa*

Kielezi *kabisa* katika (95) ni chagizo cha KH *kwa masaibu*. KH hiki chaweza kuwakilishwa katika kielelezo tungo kama ifuatavyo:




KN kinafafanua H hadi kwa H' kwa hivyo ni kijalizo lakini KE kinafafanua H' hadi kwa H' katika mchoro (95) jukumu linalotekelezwa na chagizo kwa kutumia nadharia ya X-baa.

Ingawa virai vihusishi hutumika kama chagizo ya KN na KT kuna uwezekano wa KH kutumika kama chagizo ya KH kingine. Kwa mfano:

96) Kikombe cha mama *cha dhahabu* kimepotea.

Katika sentensi (96) KH *cha dhahabu* ni chagizo ya KH *cha mama*. Chagizo hiki kinaweza kuwakilishwa ifuatavyo katika kielelezo tungo:




Katika tungo (96) KH *cha dhahabu* ni chagizo kwa kuwa kinapanua H' hadi H' ilhali KN ni kijalizo cha H *cha* ambacho ndicho kichwa cha kirai hiki.

Kirai kivumishi pia kinaweza kutumika kufafanua kirai kihusishi kwa kutoa maelezo ambayo ni ya ziada. Itokeapo hivi, KV huwa ni chagizo ya KH husika. Kwa mfano:

97) Baruti ile ililipuka kwa kishindo *kikubwa ajabu*

Chagizo hii inaweza kuwakilishwa kama ifuatavyo katika kielezo tungo:




Katika tungo (97) KV *kikubwa ajabu* ni chagizo cha KH *kwa kishindo* kwa kuwa kinapanua H' hadi kwa H'. Kihusishi *kwa* ndicho kichwa cha kirai hiki kinachojalizwa na nomino *kishindo*.

Kitenzi kisoukomo kinaweza kutoa maelezo ya ziada na ambayo si ya lazima kwa kirai kihusishi. Kitenzi kisoukomo ni kitenzi ambacho hakina uambishi wa idadi wala njeo. Hudhihirika kwa kuwepo kwa kiambishi *ku* katika Kiswahili. Ikitokea hivi, kitenzi hiki kisoukomo huwa chagizo ya kirai kihusishi. Kwa mfano:

98) Barafu yote iliyeyuka baada ya jua *kuchomoza*

Katika sentensi (98) *Kuchomoza* ni kitenzi kinachotoa maelezo ya ziada tu kuhusu KH *baada ya jua*. Hata kitenzi *kuchomoza* kikitolewa kutoka kwa sentensi KH kitakuwa kimekamilishwa na nomino *jua*. Hivyo basi kitenzi hiki kitakuwa chagizo ya KH. KH hiki kitaweza kudhihirika kwa kielelezo tungo kama ifuatavyo:




KT *kuchomoza* ni chagizo kwa kuwa kinapanua H' hadi kwa H' katika mchoro (98)

### 3.1.1.5 CHAGIZO ZA KIRAI KIELEZI

Ingawa chagizo za Kiswahili huwa vielezi au vihusishi vinavyofanya kazi kama vielezi, kirai kielezi katika Kiswahili sanifu chaweza kuwa na chagizo kinachokifafanua. Kwa mfano:

99) Mama amesema ataamka asubuhi *sana*.

*sana* ni kipashio kinachofafanua *asubuhi* na kwa hivyo ni chagizo ya kielezi cha wakati asubuhi ingawa KE kizima *asubuhi sana* ni chagizo ya KT kama inavyodhihirika katika kielelezo tungo (99) kama ifuatavyo:






Katika kielelezo tungo (99) KE *asubuhi sana* ni chagizo ya T *ataamka*. Hata hivyo ndani ya chagizo hii kuna chagizo iliyoundwa kwa E *sana* inayotoa maelezo ya ziada kuhusu asubuhi ambayo si lazima yawepo kielezi hiki kinapanua E' hadi E'.

Kishazi kitegemezi kinaweza kutumika kama chagizo ya kirai kielezi. Carnie (2013:222) kishazi kitegemezi kinaweza kufanya kazi kama chagizo kikiwa kwa nafasi inayochukuliwa na chagizo katika sentensi husika. Kwa mfano:

100) Wengine wao wanafagia vizuri *walivyoелекезwa naye*.

Katika sentensi (100) *walivyoелекезwa naye* ni kishazi kitegemezi kinachotoa maelezo ya ziada kuhusu kielezi vizuri. Kinajibu swali vizuri vipi wala si wanafagia vipi. Kwa msingi huu, kishazi hiki kitegemezi ni chagizo ya kielezi vizuri. Chagizo hiki chaweza kuwakilishwa ifuatavyo katika kielelezo tungo:



Katika mchoro(100) KE *vizuri walivyoелекезwa naye* ni chagizo ya T wanafagia nacho kishazi kitegemezi *walivyoелекезwa naye* katika tungo hili ni chagizo ya KE kwa kuwa kama ilivyodhihirika kipanua E' hadi E'.

### 3.1.2 CHAGIZO ZA VISHAZI

Awali nadharia ya X-baa ilitumika kubaini miundo ya virai vilivyoundwa kwa kategoria kileksika kama vile: N, V, T, E, H pekee. Baadaye virai vya kategoria amilifu katika vitenzi kama vile chagizo na vishazi vikaingizwa katika nadharia hii ili kusawazisha muundo. Haya yakawezesha vipashio vikubwa kama vile vishazi kuchunguzwa kupitia kwa nadharia hii (Radford 1988:62).

Aina zote mbili za vishazi (huru na tegemezi) zaweza kufafanuliwa zaidi kwa kutumia vipashio ambavyo si vya lazima. Vipashio kama vile: kirai nomino, kirai kihusishi au kirai kielezi vinaweza kutumiwa kutoa maelezo ya ziada kuhusu vishazi. Hivyo basi tunaweza kuwa na aina mbili za chagizo za vishazi ambavyo ni:

- a) chagizo za vishazi huru
- b) chagizo za vishazi vitegemezi

### **3.1.2.1 Chagizo za vishazi huru**


Kama tulivyoelezea katika sura ya pili, kishazi huru ni kishazi ambacho maana yake ni kamilifu. Kishazi huru kinaweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X-baa kama ilivyo virai vinginevyo. Kishazi huru chaweza kufafanuliwa zaidi kwa kutumia chagizo zilizo na muundo wa vishazi vitegemezi, virai nomino, virai vihusishi na virai vielezi. Katika sehemu hii tutachanganua chagizo za vishazi huru zilizo na muundo wa vishazi vitegemezi kwa kuwa uchanganuzi wa chagizo zilizo na miundo mingine kama vile muundo wa kirai nomino au kirai kielezi utafanana na ule wa chagizo za kirai tenzi.

Kulingana na Carnie (2013:222) anasema kuwa kishazi kitegemezi kinachofanya kazi kama chagizo sharti kiwe kwa nafasi ya chagizo katika kishazi huru. Kishazi kitegemezi kinachofanya kazi kama chagizo hupanua kitenzi cha kishazi huru kutoka T' hadi T'. Chagizo za kishazi huru aghalabu huwa vishazi vitegemezi vinavyotoa maelezo ya ziada katika sentensi iliyo na kishazi huru na kishazi kitegemezi hasa maelezo ya ziada kuhusu kishazi huru. Kwa mfano:

*101) Yule mgonjwa alitibiwa vizuri hadi akapona.*

*hadi akapona ni chagizo inayofafanua kishazi huru mgonjwa alitibiwa*

Maelezo haya yanaweza kudhihirika kwenye kielelezo tungo kifuatacho:



Katika mchoro (101), kishazi kitegemezi *hadi akapona* kinapanua kitenzi cha kishazi huru alitibiwa kutoka T' hadi T' na kwa hivyo basi kukifanya kuwa chagizo ya kishazi huru yule *mgonjwa alitibiwa*.


Kulingana na mawazo ya Carnie (2013) ni wazi kuwa chagizo za kishazi huru hujumlisha kipashio kinachofafanua kitenzi cha kishazi hiki na wala si kipashio kinachofafanua kishazi kizima.

### 3.1.2.2 Chagizo za Vishazi Vitegemezi

Japo vishazi vitegemezi hutumika kutoa maelezo ya ziada kuhusu vishazi huru, vishazi hivi vitegemezi vinaweza kufafanuliwa zaidi kwa kutumia aina nyinginezo za maneno. Aina hizi zinazotoa maelezo ya ziada kwa vishazi vitegemezi vyaweza kuwa chagizo za kishazi kitegemezi husika. Chagizo za vishazi vitegemezi zaweza kuwa: vielezi, kirai kihusishi au viwakilishi.

Kirai kielezi kinaweza kutumika kufafanua kishazi kitegemezi kwa kukitolea kishazi kitegemezi husika maelezo ya ziada ambayo si ya lazima. Kipashio hiki kitakuwa chagizo ya kishazi kitegemezi. Kwa mfano:

102) Mfanyikazi yule alifagia palipokuwa pachafu *sana*.




*sana* katika (102) ni chagizo ya kishazi kitegemezi *palipokuwa pachafu* hii ni kwa kuwa inapanua kitenzi cha kishazi hiki *palipokuwa* kutoka kwa T' hadi T' na ikiwa itaondolewa katika kishazi husika kishazi hicho kitasalia na maana kusudiwa.

Chagizo zilizo na muundo wa kirai kihusishi zinaweza kutumika kutoa maelezo ya ziada kwa kishazi kitegemezi. Kipashio hiki hata kikiondolewa sentensi itakuwa na maana kamili. Kwa mfano:

103) Mfanyikazi yule alifagia alivyoelekezwa *na mwajiri wake*.

Chagizo hii inaweza kuchorewa kielelezo tungo kama ifuatavyo:




*na mwajiri wake* katika (103) ni KH kinachotoa maelezo ya ziada(ambayo si ya lazima) kuhusu *alivyoelekezwa* ambacho ndicho kitenzi cha kishazi kitegemezi hiki na kinakipanua kutoka kwa T' hadi T'.

Vishazi vitegemezi vyaweza kufafanuliwa kwa kutumia chagizo zilizoundwa kwa kirai nomino chenye kiwakilishi.Kwa mfano:

104) Mwanafunzi huyu alifanya zoezi alivyoonyeshwa *nami*

Chagizo hii yaweza kuwakilishwa na kielelezo tungo kama ifuatavyo :



*nami* katika (104) ni kiwakilishi ambacho kinatoa ufafanuzi wa ziada kuhusu *alivyoonyeshwa* ambacho ni kitenzi cha kishazi husika na hivyo basi kukifafanua kutoka kwa T' hadi T' na hivyo basi ni chagizo ya kishazi hiki kitegemezi.

### 3.3 HITIMISHO

Katika sura hii, tulidhamiria kuchunguza ni viambajengo gani vinavyounda chagizo zinazotumika kufafanua virai na vishazi katika Kiswahili sanifu. Sura hii imebaini kuwa chagizo za virai na vishazi zaweza kuchukua miundo ya KN, KH, KT, KE, KV na vishazi tegemezi. Pia katika sura hii tumeonyesha kuwa kipashio cha kiuamilifu chagizo chaweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X-baa katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu ambapo tulibaini aina ya chagizo kama vile:chagizo za kirai nomino.kirai kivumishi,kirai kielezi,kirai kihusishi,kirai kitenzi na vishazi na tukatumia nadharia ya X-baa kuzibainisha. Ilibainika kuwa chagizo zilizo na muundo wa KE zaweza kutumika kufafanua KT pamoja na kufafanua KE kingine katika sentensi fulani.

## **SURA YA NNE**

### **MAJUKUMU YA THETA YA CHAGIZO**

#### **4.0 UTANGULIZI**

Katika sura ya tatu, tuliangazia aina za chagizo na miundo tofauti ya chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu. Kulingana na Carnie (2013) njia ya kudhibiti nadharia ya X-baa isizalishe sentensi ambazo si sahihi ni kuweka vidhibiti vya kileksika kwa kuhakikisha kuwa vipashio tofauti vya kileksika vimepokea majukumu ya theta. Katika sura ya nne, tutachunguza majukumu ya theta yanayowakilishwa na kipashio chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu, namna majukumu haya yanavyotolewa kwa chagizo husika na hutolewa na vipashio vipi na jinsi ugeuzaji hutokea katika sentensi ili kuhakikisha kuwa chagizo fulani imepokea jukumu la theta. Pia tutaangazia mihimili ya kigezo cha theta kinachotumiwa kutoa majukumu ya theta kwa vipashio tofauti katika sentensi hasa nomino.

#### **4.1 MAJUKUMU YA THETA YA CHAGIZO**

Uchanganuzi wa sentensi hufanywa ili kuonyesha viambajengo vilivyounda vipashio tofauti vya sentensi husika. Uchunguzi wa majukumu ya theta ya vipashio hivyo utakuwa muhimu ili kumwezesha mtumiaji wa lugha fulani kuzalisha sentensi sahihi kisarufi. Kulingana na Cowper (1992) kando na viambajengo vya virai katika sentensi, kuna mahusiano mengine muhimu ambayo yanahusu maana. Anaongezea kuwa sentensi haistahili kupuuza sehemu ya maana na kutilia maanani muundo pekee kwa kuwa maana ni sehemu muhimu inayochangia jinsi sentensi husika itakavyoundwa.

Majukumu ya theta hutolewa kwa agumenti tofauti na vipashio maalum ambavyo ni vitenzi, vihusishi na baadhi ya viambishi katika vitenzi. Kuna aina mbili za majukumu ya theta: yanayotolewa moja kwa moja na vipashio husika na yanayotolewa nje ya vipashio hivi. Chagizo ni agumenti ambayo inaweza kupokea jukumu la theta. Katika lugha ya Kiswahili, chagizo zinazoweza kupokea majukumu tofauti ya theta ni zile zinazopatikana katika kirai kitenzi na kirai kihusishi pekee kwa vile hivi ndivyo vipashio vya kipekee vilivyo na uwezo wa kutoa jukumu la theta kwa vipashio vingine kwa kuwa nomino na vivumishi havina uwezo wa kutoa majukumu ya theta kwa vipashio vingine. Vilevile, chagizo zinazoweza kupokea majukumu ya theta ni zile zilizoundwa kwa nomino au kirai nomino, kirai kihusishi, kielezi au kirai kielezi na vishazi

vitegemezi. Kuna majukumu kadha ya theta yanayoweza kuwakilishwa na chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu.

#### 4.1.1 MTENDA

Ni jukumu linalowakilishwa na nomino inayosababisha tendo au tukio fulani kutendeka. Kulingana na Cook (1989) jukumu la theta la mtenda aghalabu huwakilishwa na kiumbe chenye uhai. Katika Kiswahili chagizo kinachowakilisha jukumu hili la theta aghalabu hutokea katika kirai kitenzi na huwa na muundo wa kirai kihusishi. Kirai kihusishi hiki hutambulishwa kwa kihusishi *na* kilicho kichwa cha kirai kihusishi husika. Kwa mfano:

105) Jahazi hilo liliongozwa vyema *na Yohana*.

*na Yohana* ni kipashio ambacho ni chagizo kwa kuwa hata kikiondolewa kutoka sentensi husika sentensi hii bado itakuwa na maana kisarufi. Chagizo hiki kimeundwa kwa kihusishi *na* pamoja na nomino *Yohana*.

Jukumu hili la theta la mtenda hutolewa kwa chagizo kilicho na muundo wa kirai kihusishi kupitia kwa:hali ya kitenzi pamoja na kihusishi na.

Hali tofauti za kitenzi kimoja zaweza kuamua ni majukumu yepi ya theta ambayo kitenzi hiki kitatoa kwa agumenti zake kama vile kwa chagizo. Tukiangazia vitenzi katika kauli tenda na kauli tendwa tutapata kuwa vitenzi vya kauli tenda hutoa majukumu tofauti kwa agumenti zake na yale yatakayotolewa na kitenzi husika kikiwa katika kauli tendwa. Kitenzi *ongoza* kitatoa majukumu tofauti ya theta kwa chagizo zake kutegemea ikiwa kimo katika kauli tenda au kauli tendwa. Kwa mfano:

106) Yohana aliliongoza vizuri *jahazi hilo*.

Katika sentensi (106) kitenzi *ongoza* kinatoa jukumu la theta la mtendwa kwa chagizo *jahazi hilo* ilhali kitenzi hicho hicho kinatoa jukumu la theta la mtenda la chagizo *na Yohana* katika sentensi (105). Kinachosababisha kitenzi hiki kuweza kutoa majukumu haya tofauti ya theta kwa chagizo mbili tofauti ni hali ya kitenzi husika. Katika sentensi (106) kitenzi hiki ni kitenzi tendi ilhali katika sentensi (105) ni kitenzi tendwa.

Kihusishi *na* katika lugha ya Kiswahili aghalabu hutumika kuonyesha mtenda wa kitendo ni nani hasa kinapotumika pamoja na nomino kufafanua kitenzi. Matei (2008:62) anasema kuwa vielezi vya namna vinaweza kufafanua kitenzi kwa kuonyesha mtendaji ni nani na hutumia kiambishi *na*

ili kuonyesha anayetenda jambo hilo. Kihusishi hiki *na* hivyo basi hutoa jukumu la mtenda kwa nomino *Yohana* ambayo imo ndani ya chagizo *na Yohana*.

#### **4.1.2 MTENDWA**

Ni jukumu linaloonyesha nomino inayoathiriwa na tendo au tukio fulani. Athari inayopokelewa na nomino hii husababishwa na mtenda. Kwa mfano:

107) Mama alibariki *mtoto wake*.

*Mtoto wake* ni chagizo kinachowakilisha jukumu la mtendwa. *Mtoto wake* ndiye anayebarikiwa na *mama na* kwa hivyo anapokea kitendo *bariki* kwa njia ya moja kwa moja. *mtoto wake* ni chagizo kwa kuwa kinafafanua kitenzi *bariki* ambacho kina sifa za kitenzi kisoelekezi. Kitenzi cha aina hii hufafanuliwa zaidi na chagizo. Chagizo hiki kinawakilisha jukumu la theta la mtendwa katika sentensi (107) inayoweza kutolewa kwa chagizo hii kupitia kwa kujua maana ya kitenzi husika.

Kulingana na Cowper (1992) jukumu la theta haliwezi kubashiriwa tu kwa kuangalia muundo wa kirai nomino fulani ila jukumu fulani litatolewa kwa kirai nomino ikiwa maana ya kitenzi kinachotoa jukumu hili kitaeleweka. Baadhi ya chagizo za Kiswahili zimeundwa kwa kirai nomino na zingine ambazo zina miundo mingine aghalabu zina nomino au kirai nomino ndani yake. Maana ya kitenzi kinachotoa jukumu la theta ikijulikana itakuwa rahisi kujua majukumu ya theta yanayotolewa kwa agumenti zinazotumika pamoja na kitenzi hiki. Hii inamaanisha kuwa maana ya kitenzi itaamua kitenzi hiki kitatoa majukumu yepi ya theta kwenye vipashio tofauti katika sentensi. Kwa mfano, kitenzi *bariki* kikitumika katika sentensi sharti kitoe jukumu la mtenda kwa nomino iliyo kwa kiima pamoja na jukumu la mtendwa kwa kirai nomino kilicho katika nafasi ya chagizo. Kwa mfano katika sentensi (107) *mtoto wake* ni chagizo iliyoundwa kwa kirai nomino na imepewa jukumu la mtendwa na kitenzi *bariki* ilhali kitenzi kiki hiki kinatoa jukumu la mtenda kwa kiima *mama* katika sentensi hiyo. Hata hivyo katika utafiti huu mkazo utatiwa kwenye chagizo si kwa kiima.

#### **4.1.3 MNUFAIKA**

Kulingana na Radford (1988) hili ni jukumu linalowakilishwa na agumenti inayopata manufaa kutoka kwa tendo au tukio fulani. Cook (1989) ni jukumu linalowakilisha na nomino zenye uhai zinazoathirika na tukio fulani au tendo fulani. Aghalabu huwakilishwa na KN ua N kinachofuata kitenzi kisichoelekezi. Kwa mfano:

108) Kitabu kile kimenunuliwa *mwanafunzi yule* na *Yohana*.



*Mwanafunzi yule* katika sentensi (108) ni nomino inayowakilisha jukumu la mnufaika. Mwanafunzi yule ndiye anayepata faida kwa kununuliwa kitabu na Yohana.

Jukumu hili linatolewa kwa chagizo mwanafunzi yule na kitenzi kimenunuliwa. Limetolewa kwa chagizo kupitia kwa:maana na hali ya kitenzi

Maana ya vitenzi yaweza kuwa vitenzi ambavyo vinawakilisha wazo moja (visawe) au vinavyowakilisha majukumu yanayopingana (vinyume). Gruber (1970) anasema kuwa vitenzi ambavyo ni kinyume vinaweza kutoa majukumu tofauti ya theta kwa chagizo zinazoandamana pamoja na vitenzi hivyo. Katika lugha ya Kiswahili haya huenda yasitokee katika vitenzi vingi vilivyo kinyume kwa kuwa vitenzi hivi huweza kutoa majukumu yale yale ya theta kwa agumenti zake. Kwa mfano kitenzi *nunua* na *uza* ni vitenzi viwili ambavyo vinawakilisha mawazo mawili tofauti yanayopingana. Japo vitenzi hivi vinawakilisha mawazo mawili tofauti yanayopingana, vitatoa majukumu sawia ya theta kwa chagizo zinazoandamana pamoja navyo hasa vikiwa na muundo sawia. Kwa mfano:

109) Nyumba hiyo imeuzwa kwa *mnununuzi huyo* na Juma.

Katika sentensi (108) na (109) chagizo *mwanafunzi yule* na *mnununuzi huyo* zinatolewa jukumu la theta la mnufaika na vitenzi ambavyo vina maana kinyume.

Kitenzi kinachotoa jukumu la theta kwa chagizo chaweza kutoa jukumu tofauti kutegemea kauli ya kitenzi kinachotoa jukumu hili aidha kuwa kitenzi tendi au kitenzi tendwa. Jukumu la chagizo la mnufaika hutolewa kwake na vitenzi vikiwa katika kauli tendwa. Kwa mfano vitenzi *nunuliwa* na *uzwa* katika sentensi (108) na (109) mtawalia vinatoa majukumu ya theta ya mnufaika kwa chagizo zake kwa kuwa vimo katika kauli tendwa.

#### **4.1.4 KIFAA.**

Hili ni jukumu linalowakilishwa na agumenti yoyote inayotumika kutekeleza tendo au tukio fulani. Aghalabu huwa kifaa ambacho kisipokuwepo, kitendo kilichotarajiwa kutekelezwa hakitatekelezeka. Chagizo kinachowakilisha jukumu hili la theta huundwa kwa KH kilicho na kihusishi *kwa* katika lugha ya Kiswahili kama kichwa chake. Kwa mfano

110) Maria alipika ugali *kwa mwiko*.

*Kwa mwiko* ni chagizo kilichoundwa kwa KH na kinawakilisha jukumu la theta la kifaa kwa vile nomino mwiko ndiyo iliyotumika kufanikisha tendo la kupika ilhali kirai kihusishi kizima kwa

mwiko kinaonyesha namna ugali ulivyopikwa kwa kutumia kifaa hicho. Jukumu hili la kifaa la chagizo hutolewa kwa chagizo husika na kihusishi *kwa* katika lugha ya Kiswahili.

#### **4.1.5 MWATHIRIWA.**

Hii ni nomino inayopitia athari fulani kutoka kwa tendo au tukio na athari hii haisababishwi na mtenda. Chagizo kinachowakilisha jukumu hili la theta katika sentensi aghalabu huundwa na nomino au kirai nomino kinachotumika pamoja na kitenzi ambacho si elekezi. Kwa mfano:

111) Ugonjwa mbaya ulimlelea sana *Yohana*.

*Yohana* katika sentensi ya (111) ameathiriwa na *ugonjwa mbaya* kwa sababu ameathirika sana na ugonjwa mbaya. Nomino *Yohana* ambayo ni chagizo hivyo basi inawakilisha jukumu la mwathiriwa katika sentensi husika. Ingawa kulingana na Kuiper na wengine (2014) nomino hazina uwezo wa kutoa jukumu la theta kwa vipashio vingine katika sentensi, sentensi (111) inaelekea kuyapinga mawazo haya katika lugha ya Kiswahili kwa kuwa nomino *Yohana* imeamuliwa itapokea jukumu lipi la theta na kirai nomino *ugonjwa mbaya* na kwa hivyo tunaweza kudai kuwa kirai nomino *ugonjwa mbaya* ndicho kimetoa jukumu la theta la mwathiriwa kwa *Yohana*.

#### **4.1.6 MAHALI.**

Hili ni jukumu la theta linalowakilishwa na nomino inayoonyesha mahali ambapo kitendo kinatokea bila kuhusisha chanzo au lengo. Kulingana na Gruber (1970) jukumu la mahali aghalabu hutumika pamoja na vitenzi vya mwendo. Anavielezea vitenzi vya mwendo kama vitenzi vinavyoonyesha badiliko fulani. Kwa mfano:

112) a) Mtu huyu anatembea *ufuoni*.

b) Mtu huyo alitembea *kando ya ufuo*.

*ufuoni* na *kando ya ufuo* ni agumenti zinazowakilisha jukumu la mahali katika sentensi (112a) na (112b) na kitenzi *tembea* ni kitenzi cha mwendo. *Ufuoni na kando ya ufuo* katika sentensi (a na b) ni chagizo zilizo na miundo ya KE na KH mtawalia na chagizo hizi zinawakilisha jukumu la mahali katika sentensi husika. Jukumu hili hutolewa kwa chagizo na: vihusishi vya mahali pamwe na aina na maana ya kitenzi husika.

Jukumu hili la theta huwakilishwa na chagizo zilizoundwa na kirai kihusishi chenye maneno kama vile: *mbele ya, kando ya, ubavuni mwa, chini ya n.k.* Kwa mfano:

113) *Alifagia chini ya meza*

Chagizo *chini ya meza* ni chagizo kinachoonyesha mahali palipofagiliwa pasi kuhusisha chanzo au lengo. Jukumu hili la theta ni la kimsingi linalowakilishwa na kihusishi *chini ya* ambacho ni cha mahali. Vihusishi vya mahali katika virai vihusishi hutoa jukumu hili la theta kwa chagizo husika. Cook (1989) anasema kuwa si lazima vihusishi vya mahali viwepo katika sentensi ili sentensi iwe na chagizo kinachowakilisha jukumu la theta la mahali. Kuwepo au kutokuwepo kwa virai vihusishi kama chagizo ya kitenzi hutegemea aina ya kitenzi. Kwa mfano kitenzi *paka* kinaweza kutoa jukumu la theta la mahali kwa chagizo kikiwa na kirai kihusishi ama kirai kihusishi kisipokuwepo. Kwa mfano:

114) a) Alipaka rangi nyekundu *kwa ukuta*.

b) Alipaka rangi nyekundu *ukutani*.

Katika sentensi (114a) *kwa ukuta* ni chagizo kinachowakilisha jukumu la mahali na kina muundo wa KH lakini katika(114b)*ukutani* ni chagizo kinachowakilisha jukumu la theta la mahali na chagizo hiki hakina muundo wa KH lakini kina muundo wa KE

Kutegemea aina ya tendo linalowakilishwa na vitenzi, Gruber (1970) anaainisha kategorija tatu tofauti za vitenzi :vitenzi mwendo, vitenzi vinavyodumu na vitenzi visivyoelekeza. Kulingana naye,vitenzi mwendo ni vitenzi vinavyoonyesha badiliko la aina fulani,vitenzi vinavyodumu anadai kuwa ni vitenzi vinavyoonyesha tukio linalodumu kwa muda fulani na vitenzi visivyoelekeza ni vile vinavyoonyesha tukio linalotokea kwa ghafla. Aina hizi tatu za vitenzi huathiri majukumu ya theta yatakayowakilishwa na agumenti zitakazotumika pamoja navyo.

Vitenzi mwendo hutoa majukumu ya theta ya chanzo, lengo na mahali kwa agumenti zinazotumika pamoja navyo. Kwa mfano, kitenzi *tuma* ambacho ni kitenzi mwendo chaweza kutoa jukumu la theta la mahali kwa agumenti zake. Kwa mfano:

115) *Alinituma sokoni*

*Sokoni* ni chagizo kinachoonyesha mahali nilipotumwa bila kuhusisha chanzo au lengo. Ni jukumu linalotolewa kwa chagizo hiki na kitenzi *tuma* ambacho ni kitenzi mwendo. Kwa hivyo chagizo *sokoni* inawakilisha jukumu la theta la mahali katika sentensi (115).

Obuchi na Mukhwana (2014) wanagawa vitenzi katika aina mbili za vitenzi: vitenzi elekezi na vitenzi visivyoelekezi. Vitenzi vielekezi ni vile vinavyochukua yambwa ili viweze kukamilika kimaana na visoelekezi ni vile ambavyo havichukui yambwa kwa kuwa vimekamilika katika maana zake. Iwapo vitenzi hivi vitafafanuliwa, kipashio kitakachovifafanua kitakuwa chagizo. Chagizo zinazofafanua vitenzi visivyoelekezi vyaweza kupewa jukumu la theta la mahali na vitenzi hivi. Kwa mfano:

116) Chumo anatembea *barabarani*.

Kitenzi *tembea* katika (116) kimetoa jukumu la theta la mahali kwa kielezi *barabarani*. Kielezi hiki kinaonyesha mahali kitendo kinatokea pasi kukihusisha na chanzo au lengo.

Baadhi ya vitenzi hutegemea maana vinavyowasilisha ieleweke ili chagizo inayovifafanua ieleweke itapokea jukumu gani. Baadhi ya vitenzi huhitaji jukumu la theta la mahali litolewe kwa chagizo zinazovifafanua kwa kuonyesha iwapo mahali hapa ni ndani au nje. Kwa mfano kitenzi *weka* kitatoa jukumu la mahali linaloonyesha ndani ya kwa chagizo zinazotumika pamoja navyo ilhali kitenzi *osha* huhitaji kifafanuliwe na chagizo inayowakilisha jukumu la theta la mahali linaloonyesha mahali nje. Kwa mfano:

117) a) Chumo aliingia *ndani ya maegesho*.

b) Chumo huosha gari lake *kwa maegesho*.

Chagizo *ndani ya maegesho* katika sentensi (117a) kinawakilisha jukumu la mahali linaloonyesha mahali ambapo ni ndani ilhali katika sentensi (117b) *kwa maegesho* ni chagizo inayowakilisha jukumu la theta la mahali ambapo ni nje.

#### 4.1.7 CHANZO.

Kulingana na Habwe na Karanja (2004) jukumu hili linatekelezwa na nomino au kirai nomino kinachorejelea mahali au wakati unaoonyesha mwanzo wa kitu fulani. Naye Radford (1988) anaelezea jukumu hili kama linalowakilishwa na kipashio kinachoonyesha mwanzo wa jambo fulani aghalabu hutumika pamoja na jukumu la lengo. Jukumu hili la theta la chanzo laweza kuwakilisha na: kirai nomino (KN), kirai kihusishi (KH) au kirai kielezi (KE). Kwa mfano:

118) a) Wanafunzi hao wametoka *Kisumu* na wanaelekea Mombasa.

b) Wanafunzi hao wametoka *kwa Yohana* na wanaenda kwa Fatuma.

c) Wanafunzi hao wameanza safari *saa tatu asubuhi* na wanatarajiwa kuwasili saa kumi na mbili jioni.

*Kisumu* katika (118a) *Kwa Yohana* katika ( 118b) ni chagizo zinazowakilisha jukumu la chanzo kwa kuwa zinaonyesha mahali ambapo wanafunzi hao wanafaa kutoka katika sentensi (a) na ( b) mtawalia.

Katika sentensi (118c) sehemu iliyo katika mlazo inaonyesha wakati ambapo safari ilianza na kwa hivyo kuwakilisha jukumu la theta la chanzo hata ikiwa chagizo katika sentensi husika inaweza kuwa kishazi *saa tatu asubuhi na wanatarajiwa kuwasili saa kumi na mbili jioni* sehemu iliyokolezwa katika chagizo hii ndio inayowakilisha jukumu la theta la chanzo katika sentensi hii. Aghalabu jukumu hili hutokea pamoja na jukumu la lengo katika sentensi fulani. Jukumu hili linaweza kutolewa kwa chagizo husika na: vihusishi, aina ya kitenzi, maana ya kitenzi na viambishi vya njeo.

Jukumu hili la chanzo linaweza kuwasilishwa na chagizo zilizo na vihusishi kama vile: *kutoka, kuanzia kwa* na *kwa* katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu. Kwa mfano:

119) Wanafunzi watafagia *kutoka maktabani* hadi uwanjani.

Chagizo *kutoka maktabani* kinawakilisha jukumu la theta la chanzo kwa kuonyesha mahali tendo la kufagia linastahili kuanzia.

Katika sentensi (119) chagizo *maktabani* imepewa jukumu la theta la chanzo na kihusishi *kutoka*.

Vitenzi mwendo katika lugha ya Kiswahili hutoa jukumu la theta la chanzo kwa chagizo zinazotumika pamoja navyo. Kama tulivyoeleza hapo awali vitenzi hivi huonyesha badiliko fulani. Vitenzi vinavyoonyesha mwanzo wa badiliko linalorejelewa aghalabu hutoa jukumu la chanzo kwa chagizo zake. Kwa mfano:

120) Mtoto ametumwa dukani *kutoka nyumbani*.

Kirai kihusishi kizima *kutoka nyumbani* kinapokea jukumu la chanzo kutoka kwa kitenzi *tumwa* ambacho ni kitenzi mwendo. Kipashio hiki *kutoka nyumbani* ndicho chagizo cha sentensi (121). Hii ina maana kuwa kirai kizima kilicho chagizo ya sentensi hii kitatoa jukumu la theta la chanzo kwa kitenzi ilhali kielezi *nyumbani* kilicho sehemu ya chagizo kitatoa jukumu lili hili la theta kutoka kwa kihusishi *kutoka* kama ilivyoonyeshwa katika (120)

Kulingana na Obuchi na Mukhwana (2015:133) viambishi vinavyowakilisha njeo hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi. Viambishi hivi huwa na maumbo kama vile {na},{ta},{li} {me} nk. Kiambishi kitakachotumika kuwakilisha njeo katika kitenzi mwendo kitaathiri ni chagizo inayowakilisha jukumu lipi la theta itayotumika kukifafanua. Kwa mfano kiambishi cha wakati uliopita {li} kitatumika pamoja na chagizo iliyo na muundo kirai kielezi cha wakati kinachoonyesha chanzo lakini hakiwezi kutumika pamoja na chagizo iliyoundwa kwa kirai kielezi cha wakati kinachoonyesha lengo. Ikitokea hivyo, sentensi husika itakuwa na makosa ya kisarufi. Kwa mfano:

121) a) Bakari aliugua *jana*.

\*b) Bakari aliugua kesho

Katika sentensi (121a) jukumu la chanzo limetolewa kwa chagizo *jana* na kitenzi *aliugua* kwa kuwa kitenzi husika kina kiambishi cha wakati uliopita hata hivyo sentensi(121b) ina makosa ya kisarufi kwa kuwa kitenzi *aliugua* hakiwezi kutoa jukumu la lengo kwa chagizo *kesho* kwa sababu ya kuwepo kwa kiambishi hiki cha wakati { *li* }

Jukumu la theta la chanzo linaweza kutolewa kwa chagizo zilizo na miundo tofauti na viambishi vingine vya njeo isipokuwa kile cha wakati uliopita kama vile viambishi vya wakati uliopo {na} na vile vya hali timilifu {me}. Kwa mfano:

122) a) Juma anaanza kazi hiyo *sasa*.

b) Juma ameanza kazi hii *sasa*.

*Sasa* katika sentensi (a) na (b) ni chagizo zinazowakilisha jukumu la chanzo. Jukumu hili linatolewa kwa chagizo hii na viambishi tofauti vya njeo .Katika (a) linatolewa na kiambishi {na} cha wakati uliopo na katika( b) linatolewa na kiambishi {me} cha hali timilifu.

Maana ya kitenzi itaathiri jukumu la theta linalotolewa kwa chagizo na kipashio husika. Kwa mfano kitenzi pokea kitatoa jukumu la theta la chanzo kwa chagizo itakayotumika kukifafanua.

Mfano katika sentensi:

123) Yohana alipokea pesa *kutoka kwa Maria*.

Chagizo *kutoka kwa Maria* katika (123) ni chagizo kinachowakilisha jukumu la chanzo. Kitenzi hiki kinatoa jukumu hili kwa kuwa maana ya kitenzi pokea ni pata kitu kutoka kwa mwingine inayoonyesha chanzo na KH *kutoka kwa Maria* kinatilia mkazo mahali pesa hizi zilitoka kwa

kukifafanua kitenzi *pokea*. KH hiki ambacho ni chagizo kinapokea jukumu la chanzo kutoka kwa kitenzi linaloathiriwa na maana ya kitenzi hiki.

#### 4.1.8 LENGU

Hili ni jukumu linaloashiria mahali au wakati ambapo tendo fulani linatarajiwa kuishia. Aghalabu hutumika pamoja na chanzo. Kama vile:

124) Maria alianza safari yake saa nne asubuhi akafika nyumbani kwao *saa sita na nusu usiku*. *Saa sita na nusu usiku* ni chagizo inayoonyesha wakati ambapo tendo hili lilifikia mwisho ambalo ni jukumu la theta la lengo la chagizo hiki katika sentensi husika..

Jukumu hili la lengo huwakilishwa na chagizo zilizo na muundo wa kirai nomino, kirai kihusishi na kirai kielezi. Jukumu hili la lengo hutolewa kwa chagizo katika sentensi na vipashio vile vile vinavyotoa jukumu la chanzo ambavyo ni: vihusishi, aina ya kitenzi na viambishi vya njeo. Hata hivyo vihusishi na viambishi vya njeo vinavyotoa jukumu la lengo kwa chagizo ni tofauti na vile vinavyotoa jukumu la chanzo kwa chagizo.

Chagizo za Kiswahili zinazowakilisha jukumu hili huweza kuwa na kihusishi *hadi* kama kichwa cha kirai kihusishi husika. Kwa mfano:

125) Amenyunyuzia mimea maji kutoka saa nne asubuhi *hadi sasa*.

*Hadi sasa* ni chagizo kinachotoa ufafanuzi wa lini kitendo hiki cha kunyunyuzia kilikamilika. Jukumu hili limetolewa kwa kirai kihusishi chote na kichwa cha kirai hiki ambacho ni *hadi* kilicho na jukumu la kimsingi la lengo.

Vitenzi vilivyo na viambishi vya njeo vinavyowakilisha wakati ujao vitatumika pamoja na chagizo iliyoundwa kwa kirai kielezi kinachoonyesha wakati ambao unatarajiwa kufika na bado haujafika. Vitenzi hivi vitatoa jukumu la lengo kwa chagizo ambazo zimeundwa na kirai kielezi cha wakati hasa jukumu hili linapotokea pamoja na lile la chanzo. Kwa mfano:

126) Wasafiri walitoka nyumbani saa moja asubuhi na watafika mjini *saa kumi na mbili jioni*.

*Saa kumi na mbili jioni* ni chagizo inayowakilisha jukumu la lengo na jukumu hili limetolewa kwa chagizo hiki na kitenzi watafika. Kitenzi hiki kinatoa jukumu hili la lengo kwa chagizo mbili (mjini *na saa kumi na mbili jioni*) lakini jukumu la lengo linaloathiriwa na kiambishi cha njeo {li} ni lile la chagizo *saa kumi na mbili usiku*

Katika sehemu tofauti tumeeleza kuwa maana ya kitenzi huathiri jukumu la theta litakalotolewa na kitenzi husika kwa chagizo. Kwa mfano vitenzi vilivyo na maana ya kuelekea kwa vitatoa jukumu la lengo kwa chagizo zitakazotumika pamoja na kitenzi husika. Kwa mfano kitenzi *enda* kina maana ya elekea mahali fulani. Kitenzi hiki basi kitatoa jukumu la theta la lengo kwa chagizo zinazoambatana nacho. Kwa mfano:

127) a) Mtoto wake anaenda *kanisani*.

*kanisani* ni chagizo kilicho na jukumu la theta la lengo linalotokana na kutumiwa pamoja na kitenzi *enda*. Iwapo chagizo hiki kingetumika pamoja na kitenzi kingine chenye maana tofauti, kingewakilisha jukumu tofauti la theta. Kwa mfano:

b) Mtoto wake ametoka *kanisani*.

Chagizo *kanisani* katika sentensi (b) kinawakilisha jukumu la theta la chanzo ambalo limetolewa kwake na kitenzi *toka* kilicho na maana tofauti na kilichotoa jukumu la lengo kwa chagizo *kanisani* katika sentensi (127)

#### **4.1.9 WAKATI**

Ni jukumu linaloonyesha wakati halisi wa kutendeka kwa tendo bila kuhusisha wakati tendo lilianza au linalotarajiwa kukamilika. Kwa mfano:

128) Nimeanza kazi *leo asubuhi*.

*Leo asubuhi* ni kipashio ambacho ni chagizo kinachowakilisha jukumu la theta la wakati. Jukumu hili la theta laweza kuwakilishwa na chagizo zenye miundo ifuatayo: kirai kielezi (KE), kirai kihusishi (KH) na vishazi virejeshi. Jukumu hili linatolewa kwa chagizo kupitia kwa vipashio tofauti katika sentensi vilivyo na uwezo wa kutoa majukumu ya theta kwa vipashio vingine kama vile: vihusishi, viambishi vya njeo

Jukumu la wakati linaweza kutolewa na chagizo zilizoundwa kwa vihusishi vya wakati ambavyo havionyeshi chanzo au lengo bali vinaonyesha wakati tendo husika lilitendeka. Vihusishi hivi ni pamoja na: *baada ya; kabla ya*. Kwa mfano:

129) Ameingia *baada ya saa nne*.

Chagizo *baada ya saa nne* kinaonyesha jukumu la theta la wakati kwa kufafanua kitendo ili kuonyesha kitendo cha kuingia kilifanyika lini. Chagizo hiki hakionyeshi wakati kitendo kilianza wala kitakapokamilika ndio maana kinawakilisha jukumu la theta la wakati.



Chagizo zinazoundwa kwa kirai kielezi cha wakati na ambazo hufafanua kitenzi ambacho hakionyeshi badiliko lolote vyaweza kuwakilisha jukumu la theta la wakati. Kwa mfano:

130) Mpishi atapika chakula *saa nne usiku*.

Chagizo *saa nne usiku* kinaonyesha wakati halisi wa kupika na hivyo basi kinawakilisha jukumu la theta la wakati linalotolewa kwacho na kiambishi {*ta*} katika kitenzi *atapika*.

Baadhi ya chagizo zinazowakilisha jukumu la theta la wakati huwa na majukumu haya ya theta kama majukumu ya kimsingi ya chagizo hizi. Hii inamaanisha kuwa hata zikitolewa kwenye sentensi husika chagizo hizi zitaendelea kuwakilisha jukumu hili la theta la wakati. Hivyo basi chagizo hii haitegemei kipashio chochote katika sentensi ili kipewe jukumu la theta. kwa mfano vishazi vitegemezi vilivyo na kiambishi {*po*} cha wakati katika muundo wake aghalabu hutumika kuwakilisha jukumu la theta la wakati. Kiambishi {*po*} hutumika katika sentensi kuonyesha wakati maalum. Kwa mfano:

131) Wazazi wao walilakiwa na wenyeji *walipofika nyumbani*.

*Walipofika nyumbani* ni kishazi kitegemezi kinachoonyesha jukumu la theta la wakati. Kipashio hiki hakijahusisha chanzo wala lengo bali kinajibu swali lini.

#### 4.1.10 NGUVU

Hili ni jukumu linalotekelezwa na chagizo ambayo inajumlisha kitu kisichoonekana au kitu ambacho ni dhahania. Aghalabu katika lugha ya Kiswahili chagizo hii huundwa kwa kirai kihusishi kilicho na kihusishi *na* pamoja na nomino ambayo ni dhahania. Kwa mfano:

132) Nyumba hiyo iliangukwa *na upepo mkali*.

*KH na upepo mkali* ni chagizo inayowakilisha jukumu hili la theta la nguvu katika sentensi. Jukumu hili la theta la nguvu linawakilishwa na chagizo zilizo na virai vihusishi vilivyoundwa kwa kihusishi *kwa pamoja na kihusishi na* . Kwa mfano:

133) Alifariki *kwa ugonjwa*.

*Kwa ugonjwa* katika (133) *na upepo mkali* katika (132) zote ni chagizo zilizoundwa kwa kirai kihusishi na zinazowakilisha jukumu la theta la nguvu.

Jukumu hili la theta la nguvu linatolewa kwa chagizo husika na vihusishi ambavyo ni vichwa vya virai vihusishi ambavyo ni chagizo katika sentensi husika. Katika sentensi (132) na (133) jukumu hili limetolewa kwa chagizo na vihusishi *na* na *kwa* mtawalia.

#### 4.1.11 MALIGHAFI

Hili ni jukumu la theta ambalo hutumika kuonyesha vipashio vinavyotumika kuonyesha bidhaa ambazo zilitumika kufaulisha tendo fulani ili liwe na matokeo. Hivi aghalabu huwa vifaa vilivyotumika katika kitendo fulani. Bila vifaa hivi, tokeo la kitendo husika halingewezekana. Katika lugha ya Kiswahili jukumu hili huwakilishwa na chagizo zilizo na muundo wa kirai kihusishi. Kwa mfano:

134) Nyumba yake imejengwa *kwa matofali*.

*Kwa matofali* ni chagizo kinachowakilisha jukumu hili la malighafi katika sentensi (134). Bila matofali haya, matokeo ya kitenzi jenga ambayo ni nyumba yake hayatawezekana. Jukumu hili la malighafi linatolewa kwa chagizo na kihusishi kwa katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu.

#### 4.1.12 MAPITO

Hili ni jukumu linalowakilisha mahali ambapo nomino fulani inapitia ikielekea mahali pengine. Aghalabu jukumu hili hutumika pamoja na majukumu ya chanzo na lengo. Kwa mfano:

135) Wanafunzi hao walianza safari Kisumu, wkapitia *Nairobi* wakielekea Mombasa.

*Nairobi* ni chagizo inayotekeleza jukumu la theta la mapito katika sentensi (135). Jukumu hili linatolewa kwa *Nairobi* na kitenzi *pitia* kutokana na maana inayowakilishwa na kitenzi ambayo ni endelea na mwendo fulani. Hii yamaanisha kuwa chagizo kinachoambatana na kitenzi hiki hakiwezi kuwakilisha jukumu la chanzo au lengo.

#### 4.1.13 MATOKEO

Hili ni jukumu la theta linalowakilishwa na kipashio ambacho ni matokeo ya kitendo fulani hasa kikiambatanishwa na malighafi. Chagizo kinachotumiwa kuonyesha jukumu hili chaweza kuwa na muundo wa: kirai nomino (KN) na kirai kihusishi (KH). Kwa mfano:

136) Mama yangu ameshonea dada yangu *nguo nzuri* kwa kitenge.

*Nguo nzuri* ni kirai nomino kinachowakilisha jukumu la theta la matokeo kwa kuonyesha kuwa *nguo nzuri* ndio ilitokana na kitendo cha kushona kwa kutumia malighafi kitenge. Jukumu hili linatolewa kwa chagizo na vipashio viwili vinavyotoa majukumu ya theta. Vipashio hivi ni vihusishi na vitenzi.

Jukumu hili linaloonyesha kinachotokea baada ya kitendo fulani kukamilika laweza kuwasilishwa na kirai kihusishi kilichoundwa kwa kihusishi *hadi na kwa*. Kwa mfano;

137) Mwalimu alimchapa mwanafunzi *hadi akazirai*.

Kirai kihusishi *hadi akazirai* ni chagizo inayoonyesha matokeo ya kitendo cha mwalimu cha kumpiga mwanafunzi. Jukumu hili limetolewa kwa chagizo na kihusishi *hadi* na wala halitolewi na kitenzi *chapa*.

Maana ya kitenzi inachangia kwa utoaji wa jukumu hili la theta kwa chagizo. Kwa mfano katika sentensi (136), jukumu la matokeo la chagizo *nguo nzuri* limetolewa kwa chagizo hii na kitenzi *shona* kinachowakilisha dhana ya pitisha uzi kwa kitu ili kukiunganisha. Matokeo ya kuunganisha ni *nguo nzuri*.

#### 4.2 UTUZAJI WA MAJUKUMU YA THETA.

Baada ya kuangalia majukumu ya theta yanayotolewa kwa chagizo na vipashio tofauti tofauti na namna vipashio hivi vinatoa majukumu haya, ni wazi kuwa kila kitenzi kina majukumu ya theta ambayo ni ya kimsingi kinachopaswa kuyatoa kwa vipashio tofauti moja kwa moja. Kwa mfano kitenzi *pakia* kinatoa jukumu la theta la mtenda kwa KN ambacho ni kiima na jukumu la mtendwa kwa KN ambacho ni chagizo. Kwa mfano:

138) *Maria alipakia gari lake kando.*

KN *Maria* kinatoa jukumu la mtenda kwa kitenzi *pakia* ilhali chagizo *gari lake kando* kinatoa jukumu lake la mtendwa kwa kitenzi kile kile. Iwapo kitenzi *pakia* kitaweza kutoa majukumu tofauti ya theta kwa virai nomino vingine, au kikatoa majukumu ya theta yale yale lakini kwa nomino katika nafasi tofauti, vipashio vinavyopokea majukumu haya tofauti ya theta kutoka kwa kitenzi *pakia* vitakuwa vimefanyiwa ubadilishanaji.

Cowper (1992) anadai kuwa kila kitenzi kina majukumu mahususi ya theta kinachotoa kwa agumenti zake ikiwemo chagizo. Kwa mfano:

Kitenzi –*starehe* kitatoa jukumu la theta la mtenda kwa nomino iliyo katika nafasi ya kiima na jukumu la mahali kwa chagizo. Kwa mfano:

139) *Mama/ alistarehe/ chini ya mnazi*

Mtenda	T	mahali

Katika (139) *mama* ni mtenda ilhali *chini ya mnazi* ni mahali. Majukumu ya theta yaliyotolewa kwa agumenti hizi na kitenzi *starehe* ndiyo majukumu mahususi ya kitenzi hiki. Hata hivyo kuna

uwezekano wa kitenzi hiki kutoa majukumu tofauti na haya ya kimsingi ya theta kwa agumenti zingine kikitokea katika sentensi tofauti. Kwa mfano:

140) *Msichana huyu anastareheshwa na mpenziwe*

Katika sentensi (140) *msichana huyu* imepewa jukumu la theta la mtendwa *na mpenziwe* ni kipashio kilicho na jukumu la theta la mtenda. Majukumu haya ya kimsingi ya theta yanayotolewa na kitenzi *starehe* yamejitokeza japo yamepangiliwa kwa njia tofauti. Jukumu la theta la mtendwa limetokea kwenye kiima na lile la mtenda limetokea kwa chagizo. Hali hii inaweza kuonyeshwa kama ifuatavyo:

- i) *starehe* : <mtenda,mahali>
- ii) *stareheshwa* :<mtendwa,mtenda>

Katika (i) inaonyesha majukumu ya theta yanayotolewa kwa agumenti na kitenzi *starehe* ambayo ni mtenda kwenye kiima na mahali kwenye chagizo ilhali (ii) inaonyesha majukumu ya theta yanayotolewa kwa agumenti na kitenzi *stareheshwa* ambayo ni mtendwa kwenye kiima na mtenda kwenye chagizo.

Majukumu ya theta ya kimsingi yanayotolewa na kitenzi fulani hutolewa ikiwa kitenzi husika kimo katika kauli tenda. Iwapo kuna majukumu mengine ya theta yanayofaa kutolewa yaliyo tofauti na yale ya kimsingi, italazimu vipashio vinavyostahili kupokea majukumu haya tofauti ya theta vipangiliwe upya ili viweze kutuzwa majukumu ya theta. Mpangilio huu mpya wa vipashio katika sentensi ili vipashio hivi viweze kupokea jukumu lengwa la theta ndio tuliuita ubadilishanaji. Kwa mfano katika sentensi (140) kwa vile *KH na mpenziwe* ni chagizo inayowakilisha jukumu la mtenda, sharti *KN mpenziwe* kiwe kilibadilishiwa nafasi kutoka kwa kiima cha sentensi husika hadi kwa nafasi inayochukuliwa na chagizo. Hali hii ya kubadilisha nafasi ya *KN mpenziwe* kutoka kiima hadi kwenye chagizo inaweza kuwa ilizalishwa kama ifuatavyo:

141) *Msichana huyu alistareheshwa*\_\_\_\_\_

(*mtenda:upearaji jukumu la theta*)

\_\_\_\_\_ *alistareheshwa na mpenziwe*

(*kubadilisha kwa kupeleka KN katika nafasi ya chagizo*)

Ubadilishaji huu unapofanyika, kihusishi *na* kinatangulia *KN mpenziwe* ili kiweze kupokea jukumu la theta la mtenda. Kwa kuwa utoaji wa majukumu ya theta umedhibitiwa ili kila kitenzi

kiwe na mfumo theta mmoja, KN basi chaweza kubadilishwa kutoka mahali ambapo hakipokei jukumu la theta hadi mahali penginepo katika sentensi ili kipokee jukumu la theta

Cowper (1992) anasema kuwa ubadishanaji unaofanyiwa vipashio vya sentensi ili kuweza kupokea jukumu kusudiwa la theta sharti uwe na sifa tatu :udumishe umbo hivi kwamba unafaa usongezwe kwa nafasi ambazo zingechukuliwa na kirai nomino kingine na uwe kwenye nafasi ambapo kipashio kilichobadilishwa kitapokea jukumu kusudiwa la theta.

#### **4.3 HITIMISHO**

Katika sura hii, tumeangazia majukumu tofauti ya theta ambayo yanaweza kuwakilishwa na chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu huku tukionyesha namna vipashio tofauti hutumika kutoa majukumu haya ya theta kwa chagizo. Tumeangazia namna kipashio chagizo hubadilishwa kutoka nafasi moja katika sentensi hadi nyingine ili kukiwewezesha kupokea jukumu kusudiwa la theta.

Utafiti wetu umebaini kuwa kipashio chagizo kilichoweza kupokea majukumu haya ya theta ni kilichokuwa na miundo ya virai vielezi, virai vihusishi na virai nomino. Pia ilibainika kuwa aina ya chagizo zilizoweza kupokea majukumu ya theta ni chagizo zilizotumika kufafanua virai vitenzi na baadhi ya vihusishi. Chagizo zilizotumika kufafanua vivumishi na nomino hazikuweza kupokea jukumu lolote la theta. Ilikuwa wazi kuwa kitenzi ndicho kipashio muhimu ambacho hutoa jukumu la theta kwa vipashio vingine katika sentensi vikiwemo chagizo ingawa pia baadhi ya vihusishi hutumiwa kutoa majukumu tofauti ya theta.

Vile vile ilikuwa wazi kuwa ubadilishanaji hufanyiwa sentensi fulani ili kuweza kukipatia kipashio jukumu kusudiwa la theta. Tumegundua kuwa ili kitenzi kitoe majukumu ya theta yaliyo tofauti kwa vipashio katika nafasi tofauti, itabidi nafasi ya kipashio husika ibadilishwe katika sentensi hadi kwa nafasi itakayokiwezesha kupokea jukumu kusudiwa la theta.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.0 MUHTASARI**

Utafiti wetu umechanganua uamilifu wa chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu. Utafiti huu umeonyesha viambajengo vya chagizo katika virai na vishazi kwa kutumia nadharia ya X-baa na ukaonyesha uamilifu wa chagizo katika virai na vishazi tofauti kwa kutumia nadharia ya X-baa.

Sura ya kwanza iliweka wazi mada ya utafiti, sababu za kuchagua mada, malengo ya utafiti, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti zilizotumiwa. Sura ya pili ilifafanua vipashio tofauti vya kimsingi kama vile: virai, vishazi, kiima, kiarifu, yambwa, kijalizo na chagizo kwa kuvitolea maelezo ya kina. Sura ya tatu ilibaini aina mbalimbali za chagizo kama vile: chagizo za kirai nomino, za kirai kivumishi, za kirai kihusishi, za kirai kielezi, za vishazi huru na vishazi vitegemezi zilifafanuliwa na kuchanganuliwa kwa nadharia ya X-baa ili kubaini viambajengo tofauti vilivyotumiwa katika chagizo hizi.

Sura ya nne ilifafanua majukumu tofauti ya theta yanayotolewa kwa chagizo na vipashio tofauti katika sentensi kama vile vitenzi na vihusishi. Pia tuliangazia namna kipashio chagizo hubadilishiwa nafasi yake katika sentensi ili kiweze kupokea jukumu lililokusudiwa la theta. Tilitumia nadharia ya theta kufafanua majukumu haya ya theta ya chagizo. Sura ya tano itatoa mahitimisho ya utafiti wetu na kutoa mapendekezo.

#### **5.1 MAHITIMISHO**

Katika utafiti huu ilibainika kuwa japo chagizo ni kipashio cha kikazi kisicho cha lazima katika sentensi, chaweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X-baa. Pia tuling'amua kuwa kipashio chagizo chaweza kuwakilisha majukumu tofauti ya theta kinapotumika kufafanua kirai tenzi na kirai kihusishi lakini hakipewi majukumu ya theta kinapofafanua kirai nomino, kirai kielezi au kirai kivumishi.

Utafiti wetu ulichukulia chagizo kama kipashio cha ziada cha ufafanuzi kinachofungamanishwa na kirai chochote kile na kipashio hiki si cha lazima. Utafiti wetu ulibaini kuwa chagizo ni kipashio kinachoweza kutoa maelezo ya ziada kwa virai vyote vya kileksika kama vile: kirai nomino, kirai

kielezi, kirai kivumishi.kirai kihusishi na kirai kitenzi. Pia tuligundua kuwa chagizo chaweza kutumika kutolea maelezo ya ziada ya vishazi vikiwemo vishazi huru na vishazi vitegemezi.

Utafiti wetu ulibaini kuwa kipashio chagizo chaweza kuwakilisha majukumu tofauti ya theta yanayotolewa kwacho na vipashio viwili mahususi ambavyo ni vitenzi na vihusishi. Nomino na vivumishi havikuweza kutoa majukumu ya theta kwa kuwa kulingana na nadharia hii, vivumishi na nomino ni vipashio visivyoweza kutoa majukumu ya theta kwa vipashio vingine katika sentensi. Hata hivyo, tuligundua kuwa nomino zaweza kuathiri ni jukumu lipi la theta litatolewa kwa chagizo na kitenzi au kihusishi.

Iligunduliwa kuwa virai vielezi vingi na baadhi ya vihusishi ambavyo ni chagizo huwa na majukumu ya kimsingi ya theta yanayoweza kuvitambulisha hata ikiwa vipashio hivi vitatumika vikiwa pekee pasi kuhusishwa na vitenzi.

Hali kadhalika utafiti ulionyesha kuwa kila kitenzi kinatoa majukumu ya kimsingi kwa vipashio vingine vikiwemo chagizo hasa vikiwa katika nafasi fulani. Tuligundua kuwa ili kitenzi kitoe majukumu ya theta yaliyo tofauti kwa vipashio katika nafasi tofauti, itabidi nafasi ya kipashio husika ibadilishwe katika sentensi hadi kwa nafasi itakayokiwezesha kupokea jukumu kusudiwa la theta.

Kwa ujumla tumeonyesha kuwa kwa kutumia nadharia ya X-baa, chagizo chaweza kutumika kutoa ufafanuzi wa virai vyote pamoja na vishazi katika Kiswahili sanifu na kuwa chagizo si kipashio kinachofafanua kirai kitenzi pekee. Pia tumeonyesha kuwa chagizo hizi tofauti hasa zile za kirai kitenzi zaweza kuwakilisha majukumu mengine kadhaa ya theta ambayo ni tofauti na yale ya kimsingi ya namna,wakati,idadi na mahali.

## **5.2 MAPENDEKEZO**

Tungependekeza utafiti ufanywe kuhusu chagizo kwa kutumia nadharia nyinginezo kama vile nadharia ya uminimalisti.Mada tuliyoifanyia utafiti ilikuwa uamilifu wa chagizo katika virai na vishazi vya Kiswahili sanifu. Tuligundua kuwa baadhi ya vipashio huhitaji kuhamishwa kutoka kwa nafasi moja hadi kwa nafasi nyingine ili viweze kupokea jukumu kusudiwa la theta.

Hatukuweza kutalii uhamishaji huu kwa kina. Tungependekeza watafiti wengine wafanye utafiti kuhusu uhamishaji wa vipashio tofauti katika sentensi ili kupitisha ujumbe kusudiwa kwa kutumia nadharia nyinginezo. Vile vile vipashio amilifu vinginevyo kama vile vijalizo vya virai tofauti vyaweza kufanyiwa utafiti ili kubaini uamilifu wake katika virai hivi tofauti kwa kutumia nadharia ya theta au nadharia ya uhusika.



## **MAREJELEO**

Anderson ,J .(1971) *The Grammar of Case: Towards a Localistic Theory*.Cambridge: Cambridge University Press

Blackwell ,W. na Carnie,A. (1969) *Syntax: A Generative Introduction*.West Sussex:Blackwell Publishing Limited.

Carnie , A. (2013) *Syntax: A Generative Introduction*.West Sussex:Blackwell Publishing Limited.

Cook ,A .(1989) *Case Grammar Theory*. George-Town:George-Town university press

Cowper,E.(1992) *A Concise Introduction to Syntactic Theory: The Government Binding Approach*. Chicago:The University of Chicago Press

Culicover,P.( 2013) *Explaining Syntax:Representations,structure and Computation* Oxford United Kingdom:Oxford University Press

Gruber, J. (1970) *Studies in Lexical Relations*.Bloomington:Indiana University Linguistic club

Habwe, J. na Karanja, P. (2004) *Msingi wa Sarufi ya Kiswahili* .Nairobi:Phoenix Publishers

Haegeman, L. (1994) *Introduction to Government and Binding theory* Oxford:Blackwell Publishers

Jackendoff, R.(1977) *X Syntax: A study of Phrase structure* Cambridge: MIT press

Jerono,P .(2003) *Kishazi Huru Arifu Cha Kiswahili: Mtazamo wa X-Baa: Tasnifu ya Uzamili*: Nairobi; Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Kamau, S. (2002) *Sintaksia ya Virai vya Kiswahili Sanifu na Kikuyu cha Kabete:Ulinganishi Tasnifu ya Uzamili Nairobi: Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)*

Koech, L. (2013) *Sintaksia ya Kijalizo cha Kiswahili Sanifu: Mtazamo wa X-baa Tasnifu ya Uzamili*. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Kuiper na wengine, (2014) *Theories of Syntax Concepts and Case Studies*. New York :NY Palgrave Macmillan

Lyons, J. (1968) *Introduction to Theoretical Linguistics* New York :Cambridge University Press

Massamba, D.(2014) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar Es Salaam: TUKI

Matei, A.(2008) *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi kamili wa Sarufi*Nairobi: Phoenix Publishers

Mwachanya ,M. (2009) *Uchanganuzi wa kishazi kielezi cha Kiswahili sanifu: Mtazamo wa X-Bar. Tasnifu ya Uzamili*. Nairobi; Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Mwalili, N.(2008) *Mofosintaksia ya Kishazi Nomino cha Kiswahili Sanifu: Mtazamo wa Uminimalisti .Tasnifu ya Uzamili* Nairobi: Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Newmeyer, F .(1986) *Linguistic Theory in America* United States: Academic Press Inc

Obuchi, S. na Mukhwana, A. (2015) *Miundo wa Kiswahili: Ngazi na vipengele* .Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Olali, T. (1997) *Kikundi Nomino cha Kiswahili: Mtazamo wa Sintaksia ya 'x-bar':Tasnifu ya Uzamili*: Nairobi; Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Radford, A. (1988) *Transformational Grammar A First Course* Newyork: Cambridge University Press

\_\_\_\_\_ (1997) *Syntactic Theory and the Structure of English* Great Britian: Cambridge University press

Waihiga, G. na Kagwa, F. (2006) *Darubini ya Kiswahili* Nairobi :Phoenix publishers

Waititu ,F. na Ipara ,I, (2005) *Kiswahili Fasaha* Nairobi: Oxford university Press

Wamitila,K.W (2004) *Chemichemi za Kiswahili* Nairobi : Longhorn